# UTENDAJI KATIKA TAMTHILIA ZA SUDANA NA KIMYA KIMYA KIMYA

NA

MARY NYAMBURA KING'ORA

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YAMAHITAJI YA UZAMILI (M.A) KATIKA IDARA YA KISWAHILI CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library
0377683 8

2014.

## TABARUKU

Kazi hii naitunukia marehemu babu yangu Abraham Njihia na marehemu nyanyangu Sarah Wanjiru kwa kuniwekea msingi wa elimu.

## YALIYOMO


Ungamo .......... II

Tabaruku .......... III

Yaliyomo .......... IV

Shukrani .......... VII

Ikisiri… .......... VIII

**SURA YA KWANZA** .......... 1

1.0 Utangulizi .......... 1

1.1. Tatizo la utafiti .......... 4

1.2 Madhumuni ya utafiti .......... 5

1.3 Maswali ya utafiti .......... 5

1.4 Sababu za kuchagua mada hii .......... 6

1.5 Mipaka na upeo .......... 6

1.6 Msingi wa nadharia .......... 7

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada. .......... 11

1.8 Mbinu za utafiti .......... 17

1.9 Umuhimu wa utafiti. .......... 18

1.10 Hitimisho. .......... 18

**SURA YA PILI** .......... 19

2.0 Vipengele muhimu vya utendaji .......... 19

2.1 Utangulizi .......... 19

2.2 Maelekezo ya jukwaa .......... 20

2.3 Mandhari ... 22

2.4 Maleba ... 23

2.5 Miondoko ... 26

2.6 Uangazaji ... 28

2.7 Sauti ... 30

2.8 Kimya ... 31

2.9 Mihimili ... 32

2.10 Hitimisho ... 33

**SURA YA TATU** ... 34

3.0 Vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ... 34

3.1 Maelekezo ya jukwaa ... 34

3.1.1 Mandhari ... 35

3.1.2 Maleba. ... 39

3.1.3 Miondoko ... 40

3.1.4 Uangazaji ... 52

3.1.5 Sauti ... 55

3.1.6 Kimya ... 64

3.1.7 Mihimili ... 68

3.2 Hitimisho ... 71

**SURA YA NNE** ... 72

4.0 Vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Sudana*. ... 72

4.1. Maelekezo ya jukwaa ... 72

4.1.1.Mandhari. ... 72

4.1.2 Maleba ........ 75

4.1.3. Miondoko ........ 77

4.1.4 Uangazaji ........ 100

4.1.5 Sauti ........ 102

4.1.6. Kimya ........ 106

4.1.7 Mihimili ........ 110

4.2 Hitimisho ........ 112

**SURA YA TANO ........ 113**

5.0 Utangulizi ........ 113

5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti ........ 113

5.2 Hitimisho ........ 115

5.3. Mapendekezo ........ 115

**MAREJELEO ........ 117**

# SHUKRANI

Kiwango hiki nimefikishwa na uwezo wa Mungu. Nalihimidi jina lake. Kwa njia ya kipekee, nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Kineene wa Mutiso na Prof. Rayya Timammy. Heri msipungukiwe kamwe na rehema zake Maulana kwa kunihimiza na kunielekeza. Nawashukuru wahadhiri wangu , maprofesa: Habwe, wa Mberia, Wamitila, Kineene, Mbatiah, Abdulaziz na pia madaktari Zaja, Buregeya, Mukhwana, Olali, Swaleh na bwana Mung'ania kwa kuchangia katika ufanisi wa kazi hii.

Nawashukuru wasomi wenzangu, Ann Njoroge, Rose Kaumeuru, James Mburu, Ann Mwari, Josephine Karoki, Millicent Sabula na Simon Kilanga kwa ushirika wa kutiana ari na kuelekezana wakati wa panda shuka. Namshukuru kwa dhati Mary Ngige kwa mchango wake mkubwa katika ufanisi wa safari hii. Familia yangu na marafiki wangu wa dhati, pokeeni shukrani zangu kwa kunihimiza, kunielewa na kunitakia kila la heri. Wema wake Mola uwaandame siku zote za maisha yenu.

**IKISIRI**

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya utendaji iliyoasisiwa na Wallace Bacon ili kubainisha ikiwa tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* zimezingatia kigezo kikuu katika matini za kidrama ambacho ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani au ni majibizano ya usemi tu. Katika utafiti huu tumevitathmini vipengele vinavyochochea na kufanikisha utendaji wa tamthilia kwenye jukwaa. Maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, sauti, uangazaji, kimya na mihimili ni vipengele vya utendaji ambavyo huwawezesha waigizaji kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwenye jukwaa.

Katika utafiti wetu tumebainisha jinsi vipengele hivi vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa na pia kuutaja kwa ufupi ujumbe unaofungamana na vipengele hivi. Tumevichunguza vipengele hivi katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ya Mohamed (2011) na katika tamthilia ya *Sudana* ya Mazrui na Njogu (2006). Utafiti huu umeanza kwa somo la utafiti, kisha ufafanuzi wa vipengele vya utendaji. Pia tumevitathmini vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya.* Aidha tumevitathmini vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Sudana.*Tamati ya utafiti wenyewe inahusu muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia ufafanuzi wa mada, tatizo la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni ya utafiti na sababu za kuchagua mada hii. Vile vile tumebainisha mipaka na upeo, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na umuhimu wa utafiti. Kimsingi, tamthilia huandikwa kama hadithi fupi ya kuwasilishwa jukwaani. Licha ya kuwa tunaweza kuisoma tamthilia, ukamilifu wake ni katika kuitazama inapoigizwa jukwaani. Ni kwa sababu hii ambapo pana umuhimu mkubwa wa kuvichunguza vipengele vinavyohusika katika kulifanikisha jambo hili kwani uhusiano uliopo baina ya kazi yenyewe na hadhira una mguso zaidi kwa kuwepo waigizaji wanaoonekana.

Utafiti wetu ni kuhusu utendaji katika tamthilia. Tunarejelea tamthilia ya Mazrui na Njogu *Sudana* (2006 ) na ya Mohamed *Kimya Kimya Kimya* ( 2011 ). Utafiti wetu umejikita katika kuchanganua tamthilia hizi na kutathmini kuwepo kwa vipengele vya utendaji ambavyo huzipa tamthilia hadhi ya kuwa matini za kidrama. Vipengele hivi huziwezesha tamthilia kuwasilisha ujumbe kwa njia ya uigizaji kwenye jukwaa. Utendaji ni neno linalotokana na kitenzi tenda. Istilahi hii inahusishwa na sanaa za maonyesho na huhusisha uwasilishaji wa igizo fulani mbele ya hadhira. Mkazo wake mkubwa upo kwenye vitendo. Kuhusu utendaji katika fasihi, waandishi Madison na Hamera (2005) wanaeleza kuwa utendaji na fasihi zina uhusiano wa karibu. Utendaji ni njia tunayoitumia kuingia katika ulimwengu wa fasihi. Utendaji una midundo mingi (polyrhymic) kwani unaunganisha maneno, tajriba, hulka, udhanifu, mwili wa msomaji na matini ya kifasihi. Kulingana nao, utendaji ni dhana tatanishi.

Williams (1968) amelijibu swali la kijadi: kuna uhusiano gani kati ya matini ya kidrama na utendaji wa kidrama? Mwandishi huyu anaamini kuwa hili ni swali la kimsingi katika nadharia ya drama lakini njia pekee za kulijibu ni kuifikiria michezo kadhaa kutoka nyakati mbalimbali na kuchunguza katika kila wakati uhusiano uliopo kati ya matini na utendaji. Williams anasema kuwa anajihusisha na matini katika utendaji kumaanisha kuwa muundo wa kidrama wa kazi ambao tunaweza kuutambua tunapoisoma kazi kama fasihi hujitokeza kihalisi wakati mchezo unapoigizwa. Hivyo basi uhusiano kati ya matini na utendaji utaonekana kiutendaji. Williams pia anasema kuwa drama ni neno lenye asili ya Kiyunani 'spaua' lenye maana ya kutenda. Anaeleza kuwa neno hili linatumika kwa njia mbili kuu: kwanza kufafanua matini na pili kufafanua utendaji wa matini. Anasema kuwa drama kwa kawaida imejengwa kwa vipengele vinne; kwanza usemi unaohusisha uimbaji na ukariri, usemezano na mazungumzo. Pili, miondoko inayohusisha ishara za mikono au kichwa, midemko, vitendo vya mwili na matukio yaliyoigizwa. Tatu, usanii unaohusisha mandhari, maleba na athari za uangazaji. Nne, sauti inayohusisha muziki na athari za sauti. Elementi hizi nne hujitokeza katika utendaji. Elementi hizi nne ambazo zimetajwa na mwandishi huyu bila shaka zinaviangaza vipengele vinavyofanikisha utendaji kwenye jukwaa.

Wamitila (2002) anasema kuwa neno tamthilia limetumiwa katika upana wake kuyajumlisha maneno "drama na mchezo wa kuigiza" ya Kiingereza. Kulingana naye ni utungo unaoandikwa kwa mtindo wa mazungumzo. Anasema kuwa kuna sifa kadha ambazo hutofautisha utanzu huu na tanzu zingine. Kwanza pana matumizi ya

mazungumzo kwa upana na jukwaa huwa msingi muhimu. Pili, usimulizi wa tamthilia unategemea mazungumzo yanayokuweko baina ya wahusika mbalimbali. Usimulizi huo hutegemea pia uzungumzinafsia wa wahusika na maelezo ya jukwaani.

Wamitila (2003) anasema kuwa matendo ya wahusika hudhihirika kupitia kwa utendaji kwenye jukwaa au vionekanavyo jukwaani, kitu ambacho kinachukuliwa kuwa mhimili wa tendo fulani. Katika kazi yake ya 2008 mwandishi huyu anasema kuwa drama huwasilisha hadithi kama ilivyo katika riwaya au hadithi fupi ila tu hii huwasilishwa kwa mtindo wa mazungumzo ambao unadhamiriwa kuwasilishwa au kuonyeshwa jukwaani na waigizaji kwa kuzingatia kaida fulani za kimsingi za drama. Vilevile katika kazi hii Wamitila (2008) akimnukuu Gill (1995) anaeleza kuwa drama hurejelea sanaa za maonyesho au maigizo. Kulingana naye, fasili hii inaelekea kupuuza kuwa drama aghalabu hurejelea matini iliyoandikwa kwa maneno yanayohusishwa na wahusika wanaopatikana katika matini. Kulingana naye drama haishii kwenye utunzi tu bali pia huhusisha masuala yanayofungamana na uigizaji, uangazaji wa jukwaa, mitagusano ya waelekezi, maleba na muziki. Kwa msingi huu ni rahisi kusema drama inaanza tu baada ya kuandikwa tofauti na riwaya inayoisha tu iandikwapo. Mwanadrama anaweza kuwasiliana na hadhira kupitia kwa wahusika wake. Maoni ya wataalamu hawa bila shaka yanaafikiana hasa kuhusu umuhimu wa vipengele vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia kwenye jukwaa. Kwa maoni ya Shepherd na Wallis (2004), utendaji kwa mujibu wa sanaa hai uliibuka kutoka kwa sanaa ya uchoraji na thieta ya kimajaribio na kwamba baadhi ya wataalamu wanadai kuwa utendaji sasa umechukua mahali pa drama na thieta. Kwa mujibu wa Williams (1968), mwanadrama huandika

matini kwa njia ambayo inaweza kuigizwa moja kwa moja. Nao Griffiths na Hemming (1984) wanasema ni uwasilishaji wa matukio katika jukwaa. Wafula (2003:2) amelitumia neno drama kumaanisha somo linalohusu uigizaji wa hali fulani iwe ni vitendo, hisia au tabia za binadamu kwa kufuata utaratibu maalumu. Utendaji unahusishwa na sanaa za maonyesho na huhusisha uwasilishaji wa igizo fulani mbele ya hadhira. Mkazo wake mkubwa upo kwenye vitendo.

Wilson (1998) anatanguliza kwa kusema kuwa, wakati hadhira inapotazama na kusikiliza, waigizaji jukwaani huwasilisha maneno na utendaji wa matini katika mazungumzo yaliyobuniwa, mandhari, uangazaji na maleba ili kuleta wakati wa kipekee katika thieta.

Hivyo basi, drama ni maandishi ambayo mwandishi huwasilisha kwa madhumuni ya kusomwa na kuigizwa. Waigizaji huyatenda matendo ya wahusika jukwaani kwa njia ya maneno na ishara. Ni kazi ambayo inanuiwa kutendwa. Uchanganuzi wa tamthilia basi hauna budi kuchunguza sifa zinazohusiana na uigizaji au utendaji. Utafiti huu unahusu kutathmni mambo yanayofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa.

## 1.1 Tatizo la Utafiti

Tamthilia ni utanzu ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe wake. Hii ni kwa sababu njia inayomwezesha msanii kuwasilisha wazo lake vyema ndiyo mwafaka. Nguzo kuu ya kazi hii ni utendaji kwani matendo ya wahusika hudhihirika

kupitia utendaji katika jukwaa. Hivyo basi bila shaka kipengele cha utendaji kinachukua nafasi muhimu katika tamthilia. Ni katika msingi huu ndipo tatizo la utafiti huu ni kuchunguza ikiwa tamthilia za *Sudana,* pamoja na *Kimya Kimya Kimya,* zinaweza kudai nafasi zao kama matini za kidrama. Zinaweza kudai nafasi hii kwa kubainisha mambo yanayochochea uigizaji. Mambo haya ni maelekezo ya jukwaa, mandhari, uangazaji, maleba, miondoko, sauti, mpangilio wa jukwaa, nje ya jukwaa, kimya,vifuasi vya maleba na mihimili.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Kuna mambo au sifa zinazochochea utendaji katika matini ya kidrama na hivyo basi kuchukuliwa kama mhimili wa tendo lolote. Sifa hizo zinakuwa vigezo vya kutathmini tamthilia. Hivyo basi malengo ya utafiti huu ni;

i. Kuviorodhesha vipengele vinavyofanikisha utendaji vilivyotumiwa na waandishi wa *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* katika matini zao za kidrama.

ii. Kutathmini ufanisi wa watunzi *Mazrui* na Njogu wa tamthilia ya *Sudana* ( 2006 ) *p*amoja na Mohamed wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ( 2011) katika kuzihusisha sifa za uigizaji katika kazi zao.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

i. Je, ni vipengele vipi vinavyofanikisha utendaji vilivyotumiwa na waandishi wa tamthilia ya K*imya Kimya Kimya* na ya *Sudana* katika utunzi wao?

ii. Je, waandishi wa tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* wamefanikiwa katika kuwasilisha tamthilia ambazo zinaweza kudai nafasi kama matini za kidrama kwa kuzingatia vipengele vinavyochochea utendaji?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada Hii

Uhakiki wa tamthilia umefanywa na umeshughulikia mambo mbalimbali kama vile: nafasi ya tamthilia za kihistoria, taswira ya mwanamke, msimbo na maana kwa kuzingatia nadharia ya semiotiki, michango ya vijana kama watu wachanga waliokengeuka na kupotoka. Uhakiki huu wa awali haukuangazia uhusiano kati ya matini na utendaji ili kubainisha ikiwa watunzi husika wamezingatia vigezo au mambo ya kimsingi yanayochochea utendaji katika matini za kidrama. Baadhi ya mambo hayo yanafungamana na wahusika huku mengine yakiwa nje yao. Tumeamua kuvishughulikia vipengele hivi vinavyochochea na kufanikisha uigizaji.

Tumechagua kushughulikia mada hii kwa sababu wahakiki wa awali hawakutumia mtazamo huu katika kuzihakiki tamthilia. Katika somasoma zetu tumegundua kuwa tamthilia hizi mbili hazijahakikiwa kwa kuzingatia mtazamo huu wa utendaji. Kusudi letu hivyo basi ni kutumia mtazamo huu wa kuhakiki tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya*.

## 1.5 Mipaka na Upeo

Utafiti huu unahusu kutathmini suala la utendaji katika tamthilia ya *Sudana ya* Mazrui na Njogu (2006) na K*imya Kimya Kimya* ya Mohammed (2011). Utafiti umejikita katika

kubainisha utendaji katika matini za kidrama. Huu ni utendaji unaopatikana au kuhusiana na somo la fasihi kwani dhana hii inaweza kupatikana katika masomo anuwai na kwa hivyo ni istilahi pana na yenye kuingiliana. Matendo ya wahusika hudhihirika kupitia utendaji katika jukwaa. Yaonekanayo katika jukwaa ni muhimu katika utendaji kwani huzipa matini za kidrama uhai. Vipengele hivi ni maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, uangazaji sauti, kimya na mihimili. Hata hivyo, utafiti wetu umejifunga katika vipengele hivi tu. Hatujaingilia usanii unaohusiana na kubuni vipengele hivi. Mwongozaji wa jukwaa wakati mwingine hufikiria kuvibuni visaidizi vyake mwenyewe hata pengine asifuate vile vilivyoainishwa na mtunzi.

Uhakiki huu unazingatia kwa makini uigizaji wa tamthilia hizi na kutathmini sifa muhimu za uigizaji kwani kimsingi tamthilia huwa na wahusika, jukwaa, matendo na maagizo yanayopaswa kufuatwa wakati wa uigizaji. Kwa sababu ya upekee wa tamthilia, utafiti huu umeangazia jinsi mbinu za uigizaji zilivyozingatiwa na watunzi: Mazrui na Njogu pamoja na Mohamed. Vipengele vya utendaji ambavyo tunavitathmini ni: maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili.

### 1.6 Msingi wa Nadharia

Tunaongozwa na nadharia ya utendaji katika kuchanganua matini za kidrama na kubainisha ikiwa tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* zimezingatia kigezo kikuu ambacho ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani au ni majibizano ya usemi tu.

Kulingana na Madison na Hamera (2005) mwasisi wa nadharia ya utendaji ni Wallace Bacon aliyeishi kati ya 1914 – 2001. Alifafanua utendaji wa kifasihi kama tendo lenye msingi wake katika unyenyekevu (1984.84). Hii ni kupitia kuifanya hai stadi hii ya kifasihi kupitia uangazaji wa uwingine na wengine (otherness and others) na kuvuka mipaka ya umimi. Kwake yeye kuungana kwa stadi ya kufasiri na matini ya kifasihi ni kuvuka mipaka ya umimi ya msomaji wa tamthilia. Alisisitiza kuwa kitovu cha utendaji ni mtagusano kati ya wasomaji na matini, jambo linalostawisha kuendeleza, kubainisha na kubadilisha maisha ya ndani ya waigizaji na pia hadhira. Kwake Wallace msomaji wa tamthilia hunufaika yeye binafsi kutokana na ujumbe lakini katika uigizaji kwenye jukwaa idadi kubwa ya hadhira hunufaika kutokana na ujumbe. Tamthilia inapoigizwa katika jukwaa ujumbe huwafaidi na kuwafikia wengi na sio msomaji pekee. Madison na Hamera wanasema kuwa Bacon alisherehekea kutoa nadharia katika kazi ya utendaji wa matini za kifasihi. Aliongeza na kupanua stadi ya kusoma na kukariri usemi hadharani hadi stadi ya kufasiri na kuigiza matini ya kifasihi mbele ya hadhira.

Katika Auslander (2008), Gadamer (1986) alieleza upya uigaji. Kwake yeye uigaji unasalia sio katika matini fulani au kazi ya sanaa inayowakilisha au kuiga jambo fulani bali inahusika na watazamaji au wapokezi wa kazi wanavyotagusana na kazi hii. Tunapotagusana na kazi ya sanaa, kazi hii inatuathiri tunapogundua ukweli kupitia kuhusika kwetu katika kazi hii. Ukweli hausalii kamwe katika kazi ya sanaa inayosubiri kuvumbuliwa kupitia kufasiriwa bali huwa hai kupitia utagusano wa watu halisi na kazi kwani umimi hufichuliwa papohapo. Utendaji hivyo basi ni mchakato hai ambao hutuwezesha kufahamu mambo zaidi.

Katika Auslander (2008), Rokem (1987:179 ) analinganisha thieta na uchanganuzi wa akili. Ana maoni kuwa fikira za kibinafsi za mtu au faragha huwekwa hadharani. Hii ni kupitia usemi wa mgonjwa na mazungumzo ya waigizaji. Mawazo ya kibinafsi na ya faragha huwa halisi na wazi huku mgonjwa akihisi athari ya utakaso. Athari hii inahusishwa na hadhira ya kithieta. Katika Auslander (2008), Benjamin (1936) anasema kuwa hali ya wema au ubaya wa mtu huashiriwa na uigizaji katika utendaji halisi kwenye jukwaa.

Kwa maoni ya Madison an Hamera (2005), Wataalamu wengine ambao wanahusishwa na nadharia hii ni Robert Breen na Louise Rosenblant Kitabu cha Breen *Chamber Theatre* ni msingi katika uigizaji wa matini za kisimulizi. Hii ina maana kuwa drama pia hutumia mbinu ya usimulizi. Zipo tungo za kidrama ambazo hutegemea mbinu za kisimulizi. Wamitila (2008:279) anasema kuwa mtindo huu wa kimajaribio unahusishwa na mtunzi wa Kijerumani Bertolt Brecht. Sifa hii pia inaonekana katika tamthilia ya Mohamed, *Amezidi* ( 1995) ambayo inasisitiza ukame wa mawazo jambo ambalo linathibitisha kwamba si tamthilia zote ambazo huchimuza matendo bali zipo zinazojengwa kwenye uwazaji zaidi. Hii ni wazi kuwa matini za kidrama hazikosi vighairi vyake pia. Hata hivyo, jambo hili linazua ubishi kwa kusisitiza zaidi umuhimu wa usimulizi katika maonyesho ya ukumbini. Masimulizi sio kipengele cha pekee kilicho muhimu katika sanaa ya maonyesho.

Richard Schechner na Victor Turner kulingana na Madison na Hamera (2005), ndio waliojihusisha sana katika uendelezaji wa sanaa ya maigizo huko Marekani katika miaka

ya 1960. Schechner katika kazi yake *a*nasisitiza kwamba drama sio jambo linalotokea jukwaani tu bali ni lililojaa maana na linalotumika katika viwango vingi vya maisha ya kila siku. Alifafanua upya maana ya utendaji ambapo alipinga madai kwamba kuna mpaka uliomtenga mwigizaji mbali na hadhira. Sanaa ya utendaji hivyo basi hutilia mkazo kwenye vitendo au uigizaji ambapo watu halisi au waigizaji huchukua nafasi fulani za watu katika matini na kuigiza matendo yao kupitia mazungumzo na ishara mbele ya hadhira. Ni katika mtazamo huu tunapotambua hatuwezi kuitenga matini ya kidrama na utendaji.

Tathmini ya kifasihi kwa msomaji ni tofauti na tathmini ya yanayoigizwa. Utendaji hutusaidia kuhusika katika maisha ya matini. Sio tu msamiati bali pia malengo, utata, vinyume au uchangamani. Kushiriki kwa aina hii hustawisha ufahamu wa matini na malengo ya matini. Ufahamu huu unatuwezesha kushiriki kikamilifu katika maisha ya matini kupitia utendaji hai kama anavyoeleza Williams (1968).

Hii ina maana kuwa matini ya kidrama inapatikana kwa njia mbili ambazo ni matini andishi na matini tendaji. Katika uigizaji, mwigizaji ambaye ni mtu halisi anawakilisha mhusika au mwili wa kubuniwa ulio katika matini. Hivyo basi baina ya mwandishi, matini, mhusika na hadhira, mwigizaji ndiye huathiri katika tamthilia. Tendo la kidrama hufungamana na usemi wa kidrama.

Ni bayana kuwa matini ya kidrama na utendaji hutegemeana. Hata hivyo vighairi havikosi kwani pana uwezekano wa kuwa na drama au utendaji bila ya kuwa na matini iliyoandikwa. Kwa upande mwingine, matini ya kidrama huwasilisha ujumbe vyema

zaidi kupitia uigizaji wake katika jukwaa. Ni katika msingi wa maelezo haya ndipo nadharia ya utendaji ni mwafaka katika kutathmini utendaji wa matini za kidrama kwenye jukwaa. Kama anavyodai Bacon (1984) katika Madison na Hamera ( 2005) kuwa hadhira kubwa hunufaika kutokana na uigizaji, hivyo basi nadharia ya utendaji inafaa katika kuvitathmini vipengele vinavyofanikisha na kuleta ukamilifu katika uigizaji.

Hivyo basi nadharia ya utendaji inashughulikia kuifanya hai fasihi. Ni vigumu kufanya hivyo bila kuhusisha vipengele vinavyochochea utendaji. Ndipo tumeamua kutumia nadharia hii ya utendaji kuhakiki utendaji katika tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.* Nia yetu ni kutathmini ikiwa vipengele vya utendaji vinajitokeza katika kazi hizi. Ni lengo letu pia kutathimini ikiwa tamthilia hizi mbili zinaweza kudai nafasi kama matini za kidrama kwa kuvizingatia vipengele vinavyochochea utendaji kwenye jukwaa.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada.

Tamthilia ya Kiswahili imehakikiwa na wahakiki wengi katika kazi zao hivyo basi uhakiki wa tamthilia hauna kikomo kwa sababu wahakiki huwa na mitazamo na misimamo tofauti kuhusu kazi moja. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa utendaji sasa umechukua nafasi ya drama na thieta. Wanasema kuwa utendaji na fasihi zina uhusiano wa karibu. Utendaji ndio unatuwezesha kuingia kwenye kazi ya kifasihi.

Mohammed (1995) anaeleza kuwa vijengo vya tamthilia hutegemea mno kwa nini tamthilia hutungwa na vipi huwasilishwa kwa hadhira. Suala vipi huwasilishwa lahitaji ufafanuzi zaidi. Tofauti na riwaya na hadithi fupi, mbinu za kujieleza katika tamthilia

zinahusu pande mbili. Upande wa mwandishi na upande wa mwigizaji. Mwandishi anahitaji lugha tu katika maandishi yake kuwa njia ya kujieleza, lakini mtendaji anahitaji lugha na mambo mengine yaliyoko nje ya lugha. Katika msingi huu, jambo zima la tamthilia linahusu mambo yafuatayo; taarifa ya kisanaa, uhusika, visaidizi, maelekezo ya jukwaa, miondoko, ploti, maana na migogoro na pia wiano na hadhira hai.

Kazi hii ni ya msingi wa kutuwezesha kuzichambua tamthilia husika kwani mambo yaliyoorodheshwa yatakuwa vigezo. Tofauti ni kuwa yeye amezungumzia vipengele vya uigizaji kijumla. Sisi tutavishughulikia kwa undani katika kazi maalum ambazo ni tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya.*

Griffiths na Hemming (1984) wameziita sifa hizi zinazofanikisha uigizaji ishara za kidrama (dramatic signals) nazo ni mpangilio wa jukwaa, mandhari, miondoko, viashiria (symbols), maleba, maelezo kwa hadhira, muziki, uangazaji, maelekezo ya jukwaa, nje ya jukwaa na kimya. Vipengele hivi ni mwafaka katika utafiti wetu kwa sababu vinatuelekeza kwenye mambo tunayotathmini ingawa sisi tutavichunguza kwa kina na katika kazi maalum.

Maoni ya Wilson (1998) ni kuwa waandishi wa tamthilia wanaelewa vyema kwamba yanayowasilishwa katika jukwaa ni tofauti na tunayowaza baada ya kusoma matini. Bila shaka athari itakuwa tofauti. Mambo kama mandhari, mazungumzo na maleba yanaathiri utendaji na waigizaji vile vile. Jinsi waigizaji wanavyofasiri majukumu yao kama vile ishara za uso, miondoko na toni ni mambo yaliyo na athari kubwa. Wilson pia anasema

kuwa utendaji unatokana na kujumlishwa kwa nguvu kadhaa au mambo mengi. Mengine ni dhahiri na mengine si dhahiri. Mambo haya yanahusisha waigizaji, rangi, maleba, mandhari na pia maoni na hisia zinazowasilishwa katika matini. Sifa hizi bila shaka zitatuongoza katika kutathmini ikiwa tamthilia za S*udana* na *Kimya Kimya Kimya* zimefanikiwa kuwa na sifa zinazofanikisha uigizaji kwenye jukwaa. Tofauti ni kwamba mwandishi huyu amevitaja vipengele vinavyochochea uigizaji kwa jumla ilhali sisi tunavichunguza kwa undani na katika matini maalum.

Wamitila (2008) anasisitiza kuwa drama au kazi ya maigizo huandikwa kimsingi ili iwasilishwe mbele ya hadhira. Kulingana naye, hali hii inatukumbusha kuwa ni muhimu tunapozichunguza matini za kidrama kuangazia ikiwa zina unyumbufu wa kiasi gani. Kutokana na sifa ya uhai inayohusishwa na kazi hii, sifa muhimu zinazorejelewa ni: jukwaa, ishara za mikono, lugha, toni ya maneno ya wahusika, ishara uso, mbinu za ubainishaji na ukuzaji wa wahusika, mazingira, upodoaji, maleba, uangazaji, sauti, nyimbo, muziki na ngoma. kazi hii ni mwafaka kwetu kwa sababu imedokeza vipengele vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa. Tofauti ni kwamba sisi hatushughulikii toni ya maneno ya wahusika, ubainishaji na ukuzaji wa wahusika na upodoaji.

Musyoka (1996) ameshughulikia uhakiki wa fani katika tamthilia za Jay kitsao. Ameshughulikia umbuji na wahusika, uhusika, ploti na matumizi ya lugha kwa kurejelea tamthilia za Jay Kitsao. Utafiti huu utakuwa kirejelezi kwetu hasa umbuji wa wahusika kwa sababu ufanisi wa uigizaji hai katika kuwasilisha ujumbe kwenye jukwaaa

unategemea wahusika walivyoumbwa pamoja na vipengele vya kuchochea uigizaji. Tofauti ni kwamba kazi yetu inashughulikia vipengele vinavyowawezesha waigizaji kuweza kuigiza nafasi za wahusika ili kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa huku tukizirejelea tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.*

Waihiga na Kamau (2002) katika mwongozo wa *Kilio cha Haki* wameeleza muhtasari wa kila onyesho. Wamebainisha wahusika na sifa zao. Wanasema kuwa katika kazi ya fasihi, mwandishi hutumia wahusika kwa njia mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe walio nao. Mtunzi huongea na hadhira yake kupitia kwa wahusika aliowaumba. Huwatumia wahusika kupitisha yaliyo moyoni mwake kwa wasomaji, watazamaji na wasikilizaji wa kazi yake. Vile vile wameangazia usawiri wa wahusika na vile wanavyochangia katika kukuza dhamira na maudhui ya tamthilia ya *Kilio Cha Haki.* Kazi hii itatufaa katika uchanganuzi wa vipengele vinavyowawezesha waigizaji wanaochukua nafasi za wahusika kama hawa kufanikiwa katika kupitisha ujumbe kama wa mtunzi huyu kupitia uigizaji katika jukwaa. Tofautti ni kwamba sisi tunatathmini matumizi ya vipengele vya uigizaji katika tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya.*

Were (2012) amechunguza fani katika tamthilia ya Kiswahili huku akirejelea tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Kijiba cha Moyo.* Mhakiki huyu amechanganua vipengele vinne vya fani ambavyo ni ploti, wahusika, dayalojia, na monolojia kwa kuonyesha jinsi vinavyojenga kazi nzima. Uhakiki wetu unashughulikia vipengele vinavyowawezesha wahusika kudhihirisha hisia zinazotokana na ishara za nyuso zao wanapozungumza jukwaani na hivyo basi kazi hii ni mwafaka kwetu. Tofauti ni kwamba sisi

tumevitathmini vipengle vya uigizaji katika tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya.*

Mwenderani (2012) ameshughulikia taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kiswahili. Mada yake imetathmini taswira ya mwanamke kwa kurejelea tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Pango* ili kujua ikiwa mwanamke wa kisasa amefikia hali ya kujikomboa katika ulimwengu wa kisasa. Kazi hii inatufaa kwa sababu taswira hii ya mwanamke inaweza kudhihirika kwa kuwasilishwa kwenye jukwaa. Vipengele vya utendaji tunavyochunguza ndivyo vinavyohusika na kuleta ufanisi katika uwasilishaji kwenye jukwaa. Tofauti ni kwamba kazi yetu imeshughulikia vipegele vinavyowawezesha waigizaji kuuwasilisha ujumbe wa aina hii kwenye jukwaa na tumezirejelea tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.*

Kisiroche (2008) ameihakiki tamthilia ya *Zilizala* kwa kushughulikia sauti ya mwanamke dhidi ya ubabedume. Ameangalia nguvu ya hoja ya mwanamke na mbinu nyingine walizotumia wahusika wa kike katika tamthilia hii katika harakati zao za kuupiga vita ubabedume. Ujumbe muhimu kama huu unaweza kubainika vyema kwa kuwasilishwa kwenye jukwaa kwa kuzingatia vipengele vinavyochochea utendaji. Kazi hii inatufaa kwani tunachunguza vipengele vinavyowawezesha waigizaji kufanikiwa katika kuwasilisha ujumbe wa aina hii kupitia uigizaji kwenye jukwaa. Hata hivyo, utafiti wetu umezitathmini tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.*

Mutswenje (2012) ameshughulikia nafasi ya tamthilia za kihistoria katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea tamthilia za *Kinjeketile* na *Mzalendo Kimathi.* Amechunguza thamani ya tamthilia hizi za kihistoria katika fasihi ya Kiswahili. Kazi hii ina manufaa kwetu kwani maswala haya ambayo ni muhimu sana kwa jamii yaweza kubainika vyema kwa wengi kupitia uigizaji. Vipengele vya uigizaji tunavyovishughulikia huleta ufanisi katika utendaji. Tofauti ni kwamba sisi tunatathmini matumizi ya vipengele vinavyofanikisha utendaji katika tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya.*

Kiongera (2012) ameshughulikia mchango wa vijana kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia teule za Kiswahili. Ameliangazia swala la mahusiano na mchango wa vijana katika kuyatatua matatizo yanayozikabili jamii kwa kurejelea tamthilia za *Kifo Kisimani*, P*ango*, *Maua kwenye Jua la Asubuhi* na *Seserumbe.* Swala kama hili lenye umuhimu katika jamii linaweza kuangaziwa vyema zaidi kwa kuwasilishwa kwenye jukwaa huku utendaji ukichochewa na vipengele vya utendaji. Sisi kwa upande wetu tunajihusisha na vipengele hivi vinavyofanikisha uigizaji wa ujumbe kwenye jukwaa ila tathmini yetu inahusu tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya.*

Mukobwa (1985) amejadili maudhui ya tamthilia tano za Hussein E *Kinjeketile, Wakati Ukuta*, *Alikiona*, *Mashetani* na *Arusi.* Kazi hizi zinazungumzia masuala ya utamaduni, uadilifu, siasa na uchumi. Kazi hii ni mwafaka kwetu kwani masuala muhimu kama haya yanaweza kuifaidi jamii kwa kuwasilishwa vyema kwenye jukwaaa kupitia vipengele vya uigizaji ambavyo sisi tunavishughulikia. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa sababu sisi

tunachunguza mambo yanayofanikisha utendaji katika tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.*

Wafula (2003) katika uhakiki wa tamthilia ameshughulikia mgongano wa utamaduni katika *Wakati Ukuta* na *Hatia.* Utafiti wetu ni tofauti na huu kwa sababu unanuia kuchanganua vipengele vinavyochochea na kufanikisha utendaji kwenye jukwaa kwa kuzirejelea tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya.* Hata hivyo, mgongano kama huu wa tamthilia unaweza kuwasilishwa kwa njia ya mazungumzo na matendo kwenye jukwaa na kuwa na athari kubwa kwa hadhira kwa kuchochewa na vipengele vya utendaji ambavyo tunashughulikia kwa

Kazi hizi zote zimetoa maelekezo kuhusu vigezo vya utendaji. Kwa ujumla, uhakiki wa tamthilia wa awali umezingatia zaidi ufafanuzi wa maudhui na masuala ya mtindo na miundo mbalimbali. Katika utafiti huu tumetathmini utendaji katika tamthilia ili kubainisha ikiwa utanzu huu unapotungwa hutarajiwa kuigizwa kwenye jukwaa ili matukio yadhihirike kwa hadhira.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu unahusu vipengele vinavyofanikisha uigizwaji katika tamthilia. Ili kutekeleza utafiti huu, tumejikita katika kusoma tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya* ili kutathmini vipengele vinavyofanikisha utendaji kwenye jukwaa. Katika maktaba tumesoma kazi zinazohusiana na mada hasa zinazogusia vipengele vya utendaji katika fasihi hasa katika tamthilia. Vilevile tumerejelea mtandao kutafuta habari mwafaka

zinazohusiana na nadharia ya utendaji katika fasihi. Tumerejelea makamusi maalumu ya fasihi pia ili kuweza kubainisha vipengele vinavyohusiana na utendaji. Tumezungumza na wataalamu wanaofundisha drama na tumezisoma matini zingine za kidrama ili tupate msingi thabiti wa kuzitathmini tamthilia husika.

### 1.9 Umuhimu wa Utafiti.

Utafiti huu ni msingi kwa wahakiki wa baadaye kwani wataweza kuitumia kazi hii kama kirejelezi. Utafiti huu pia ni msingi kwa uhakiki wa baadaye wa tamthilia kwa sababu uhakiki uliotangulia haujatumia mtazamo huu. Kazi hii pia ni kielelezo kwa wasomaji wa tamthilia na wapenzi wa sanaa ya maigizo kwa kuwa inaangazia vipengele vinavyochochea na kufanikisha utendaji au uigizaji.

### 1.10 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza tumeshughulikia utangulizi, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, mipaka na upeo, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti na umuhimu wa utafiti. Katika sura inayofuata tumevifafanua vipengele vinavyochochea uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa ambavyo ni maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, uangazaji, miondoko, sauti, kimya na mihimili.

# SURA YA PILI

## 2.0 Vipengele Muhimu Vya Utendaji

### 2.1 Utangulizi

Katika utafiti huu tumeangazia mambo yanayochochea uigizaji katika tamthilia. Huu ni utanzu ulio na sifa za kipekee na ulio na vipengele vinavyofanikisha uigizaji na kuutofautisha utanzu huu na tanzu zingine za fasihi andishi kama vile riwaya, ushairi na hadithi fupi. Stadi za utendaji wa tamthilia ni stadi ngumu zinazohitaji mafunzo maalumu na ya muda mrefu. Tamthilia ni utanzu mmojawapo kati ya tanzu kuu za fasihi andishi. *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2004:272) inaeleza kuwa tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazumgumzo. Wafula (2003:10) anaieleza dhana hii kama moja kati ya tanzu kubwa na muhimu za fasihi.

Huu ni utanzu ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe. Ni utanzu ambao huandikwa kwa mtindo wa mazungumzo ya wahusika. Hivyo basi kigezo kikuu ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani kama sanaa ya utendaji. Maelekezo ya jukwaa, miondoko, mandhari maleba, uangazaji, sauti, kimya na mihimili ni vipengele ambavyo vina nafasi kubwa katika tamthilia. Utafiti huu unanuia kutathmini ikiwa Mazrui na Njogu (2006) na Mohamed (2011) wamefanikiwa katika kuwasilisha tamthilia zao kuigizwa jukwaani kwa kuzingatia vipengele vya utendaji.

Griffiths na Hemming (1984:100) wanasema kuwa ni vigumu kuvishughulikia vipengele kwa kuviainisha kwa sababu vinapishana nafasi. Kwa mfano mandhari, maleba, uangazaji, sauti, toni, miondoko na kimya kujitokeza katika maelekezo ya jukwaa. Vilevile mihimili hujitokeza kwenye mandhari.

Mwandishi wa tamthilia mwenyewe hutumia maelezo ya ziada kwenye taarifa ya tamthilia kusaidia kupambanua sifa, tabia na saikolojia za wahusika wake. Uhusiano wa tamthilia kwa hivyo si ule unaoonyeshwa kwa vivuli vifu au wahusika wasiotenda katika maandishi tu bali ni matokeo ya pamoja baina ya vivuli vifu vya maandishi vinavyotiwa uhai kwa kugeuzwa kuwa viumbe halisi vinavyotenda katika jukwaa kama anavyoeleza Mohamed (1995)

**2.2 Maelekezo ya Jukwaa**

Mbatia (2001) anaeleza kuwa haya ni maelezo katika tamthilia ambayo huwa yameandikwa kwa hati mlazo na kuwekwa kwenye mabano juu ya miondoko ya wahusika, matendo yao na ishara wanazofanya. Maelezo kama haya pia yanatoa picha ya mandhari ya jukwaa.

Mohamed (1995) anaeleza kuwa, ili maana ya taathira ya kisanaa iwe kamili, sehemu ya maelezo ya jukwaa ni muhimu sana katika tamthilia yoyote ile. Umuhimu huu unatokana na kwamba katika tamthilia hakuna maelezo ya mandhari, mavazi na nyakati mbalimbali za uhai wa kadhia yote ya tamthilia. Kwa mfano tamthilia yenye kadhia ya miaka hamsini nyuma lazima ihitaji maelezo ya vifaa, samani, mavazi na mapambo aina

nyingine kabisa tofauti na wakati huu. Pili, katika tamthilia hakuna maelezo na simulizi tunazozikuta kwenye riwaya na hadithi fupi bali kuna utendaji unaosimamia maelezo na simulizi. Hivyo basi hali hii inalazimu kuwepo maelezo ya jukwaa yanayoshughulikia vifaa, samani, mavazi, mapambo, mazingira na hata matendo ya wahusika. Maelekezo ya jukwaa yanaipa tamthilia maweko ya kipahala kama vile shamba, mjini, nje, ndani, mahakamani na pia ya kiwakati na kiuchumi kama vile kuonyesha maisha ya kitajiri na kimaskini kwa ajili ya kuimarisha maana na madhumuni ya tamthilia.

Kwa ujumla, maelekezo haya hutoa maelezo kuhusu mienendo na miondoko ya wahusika, hutoa maelezo kuhusu wasifu wa wahusika kama vile mavazi, lugha na ishara uso. Pia hutoa maelezo kuhusu mandhari au mahali pa mchezo, hufafanua mazingira na hata maleba ya wahusika, hutoa vielekezi vya jinsi ya kuandaa jukwaa kwa ajili ya uigizaji, hutoa maelekezo ya jinsi ya kutumia na mchango wa viambata jukwaa vingine. Wamitila (2002) anasema kuwa maelekezo ya jukwaa huwa na dhima kubwa katika kazi ya kidrama. Kimsingi, maelekezo haya hutudokezea mandhari, wakati, matendo, ujaji na uondokaji wa wahusika, sifa za jukwaa, maleba na mengine.

Kipengele hiki cha maelekezo ya jukwaa kinasaidia kukamilisha maana ya tamthilia. Baadhi ya tamthilia huwa na maelezo ya jukwaa ambayo ni marefu kutegemea jukumu lake. Maelekezo ya jukwaa yanatumia lugha ya nathari na ndio yanachukua mtindo wa kisimulizi wa riwaya. Kwa kiasi kikubwa, maelekezo ya jukwaa yanamwezesha mwanatamthilia kuwa na nafasi ya kutumia mbinu ya kinathari na hasa pale ambapo anawaelezea wahusika wake na mawazo yao fulani. Njia hii ya kimaelezi au kinathari

inamwezesha mwanatamthilia kuyasawiri mandhari au hali vizuri na kwa ukamilifu. Maelekezo ya jukwaa huwa na athari kubwa kwenye kazi nzima na kwa kiasi kikubwa tamthilia itaathirika sana yakikosekana.

## 2.3 Mandhari

Mbatia (2001) anasema kuwa istilahi hii inahusiana hasa na utanzu wa drama na inarejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yaliyoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Pia anasema kuwa istilahi mandhari hutumiwa kwa maana ya sura ya mahali, hasa ikiwa ya kuvutia.

Wamitila (2011) anasema kuwa mandhari hutumiwa kueleza sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili huweza kutumiwa kwa mapana kueleza pia mazingira ya kisaikolojia ya tendo fulani. Mandhari huweza kurejelea yale mazingira ya jukwaani na hata wakati wenyewe.

Wamitila (2002) anasema kuwa matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi ya kifasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalum. Hiki ndicho kinachoelezwa kama mandhari. Ni ile arki au elementi ambayo hutufichulia wapi na lini ambapo matukio fulani yalifanyika. Neno hili hutumiwa kurejelea wakati na sehemu ambapo matukio ya msuko hutokea. Mathalan mandhari huathiri sana mkondo wa kimaudhui na huwa na athari kubwa kwenye dhamira kuu ya kazi husika. Sio lazima yawe ya kihalisia au kijiografia.

Anasema kuwa mbinu ya kurefusha mandhari (distancing) huweza kutumika kama ilivyofanyika katika riwaya ya Shaaban R (1951) *Kusadikika* ili kujiepusha na uwezekano wa kushambuliwa. Mandhari yanakuwa muhimu kutokana na mchango wake katika kuwapa wahusika wasifu fulani. Mazingira anamojikuta mhusika yanaathiri kwa kiasi kikubwa wasifu wake kama mhusika au sifa alizonazo.

Griffiths na Hemming (1984) wameeleza kuwa wasomaji wasiokuwa na tajriba katika drama mara nyingi hutatizika kupata taswira ya mchezo (visualizing) kichwani. Hii ni kutokana na kupuuza maelezo ya jukwaa na pia kujishughulisha na wahusika na usimulizi. Ni muhimu sana kuzingatia mandhari. Hadhira katika thieta huona na kuamua papo hapo. Wao hushawishika na kutoa hukumu mara tu mandhari yanapoonekana.

Haya yanadhihirika kwa kuangalia mfano huu:

> *Asubuhi uwanjani, viti vimepangwa vizuri katika kibanda chenye kivuli, Nyuma ya kibanda vilima vinaonekana.*(uk.1)
>
> Mberia, K. ( 2001)

Maelekezo haya ya jukwaa yanaeleza mazingira na sura ya mahali maalum pa uigizaji na pia kudokeza wakati wa uigizaji.

## 2.4 Maleba

Kuna tofauti muhimu kati ya mavazi ya maisha ya kila siku na maleba katika jukwaa. Maleba huwasilisha ujumbe sawa na ule wa mavazi ya kawaida kwa kuzingatia jinsia, nafasi na jukumu. Lakini katika jukwaa ujumbe unavyazwa kwa sababu kila elementi

katika jukwaa inaangaziwa. Mbatia (2001) anafafanua maleba kama mavazi maalumu yanayotumiwa na waigizaji kubuni taswira ya watu wanaoigiza au wahusika.

Wamitila (2011) anasema kuwa maleba ni mojawapo ya vipengele muhimu vya mandhari. Maleba yanayotumiwa na wahusika wa kazi za kifasihi yana mchango mkubwa kwenye athari ya tamthilia nzima. Maleba haya huweza kuakisi kipindi cha kihistoria pamoja na hali iliyokizunguka kipindi hicho. Uteuzi wa maleba hudhibitiwa na nia ya kutaka kuizua athari fulani. Maleba pamoja na mafigu au vinyago vya wahusika huweza kutumiwa kuwapa wahusika sifa ambazo sio za binadamu wa kawaida hivyo basi kufanikisha utendaji.

Kuhusu maleba, Griffiths na Hemming (1984:107) wanaeleza kuwa kipengele cha drama ambacho mara nyingi humkwepa msomaji ni cha maleba. Hata ikiwa amemudu stadi au mazoea ya kufuatilia maelekezo ya jukwaa, yeye hukosa kuona umuhimu wa maleba fulani yaliyoagizwa na mtunzi wa tamthilia. Ni jambo la kushangaza kuwa ingawa katika maisha ya kila siku tunakuwa wepesi katika kuhukumu wenzetu kutokana na jinsi walivyovalia, tunapowatazama waigizaji katika jukwaa tunapuuza jambo hili. Pengine au huenda ikawa sababu ni kuwa tunatarajia waigizaji ni sharti wavalie au ni kawaida yao kuvalia. Changamoto zaidi hutokana na wazo kuwa maelekezo ya maleba wakati mwingine huwa hayajajitokeza katika matini.

Wilson (1998:387) anasema kuwa kwa sababu yanavaliwa kiuhalisia na waigizaji, maleba ndicho kipengele cha kipekee cha vitu vionekanavyo katika jukwaa. Waigizaji na

maleba huchukuliwa kama kitu kimoja, huungana na huwa sura moja katika jukwaa. Vilevile maleba yana thamani ya kipekee. Huongeza kipima rangi, umbo, msokotano na uashiriaji kwa athari nzima. Maleba yana uhusiano wa karibu na vifuasi kama vile vipodozi, mapambo ya mwili kama vile mikufu na bangili, mitindo ya nywele, mafigu na nywele bandia. Maleba yana uwezo wa kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira fauka ya kupendeza.

Kwa mujibu wa Aston na Savona (1991:134) maleba hubainisha picha halisi ya mhusika na vilevile tabaka lake na huweza pia kutumiwa kuashiria, kufanana au kutofautiana. Maleba pia hutofautisha kati ya wahusika wa kike na wa kiume.

Mambo haya yanabainika katika mifano hii:

> (…*Wafungwa sita waliovaa nguo nyeupe zenye namba kubwa kifuani na mgongoni…*) ( uk.1.) (… *Amevaa mawani. Ana mvi chache kichwani na ana ndevu za kubabaisha kama za beberu. Kifuani amevaa shati jeupe na tai nyeusi…*) ( uk.9.)
>
> (… *Mawaziri wake wamevaa kama yeye. Magwanda mapana na makaptula makubwa.. Mkulima amevaa shuka kiunoni na fulana iliyotatuka… wote wana vitambi isipokuwa… viatu vya matairi vya Rais…*) ( uk.27)
>
> Kezilahabi, E. ( 2009)

Mavazi ya wafungwa yanawatambulisha. Magwanda mapana na makaptula makubwa yanayopwaya yanadhihirisha hadhi ya viongozi ambao hawatekelezi wala kuyamudu majukumu yao iwapasavyo. Mavazi ya mkulima yanadhihirisha umaskini.

Mavazi na vifuasi vya mavazi yaliyovaliwa na wahusika yanafanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia hii kwenye jukwaa.

## 2.5 Miondoko

Mohamed (1995) anasema kuwa hii ni stadi ya utendaji inayohusiana na vipi mwili na viungo vya mtendaji kama vile mwili na viungo vya mikono, miguu, macho, kope na nyusi zinavyoondoshwa na kusogezwa katika hali nzima ya utendaji. Watendaji hulazimika kutumia ishara za viungo vya mwili hasa mikono na hisia za uso kuonyesha ucheshi, huzuni, hamaki, kejeli, ukatili, imani, maumivu, mshangao na hata wasiwasi. Miondoko inasaidia pia kujenga ukamilifu wa kimaana na kisanaa hasa pale mhusika katika miondoko anapoiga wasifu, tabia na matendo kwa mujibu wa umri, cheo, uke uume na kadhalika. Mambo kama maumivu, msiba, furaha na misukumo ya hisia mbalimbali huhitaji ufundi mkubwa wa miondoko. Baadhi ya miondoko huoanishwa na mwandishi katika maelezo ya jukwaa lakini mengine hukamilishwa na mwigizaji au mhusika. Kila wakati katika tamthilia tunakutana na maneno kama akakaa, wakacheka pamoja, wanaitikia kwa vichwa kwa mgutuko na anakwenda kama mgonjwa. Hizi zote ni aina mbalimbali za miondoko inayojaribu kusaidia kupatikana maana ya matini.

Griffiths na Hemming (1984: 104) wanaeleza kuwa hali ya kuonekana ya drama katika jukwaa huwezesha miondoko kuwa na athari kubwa. Wahusika kuweza kusonga kwa ustadi hadi neno lililosemwa likastawishwa au kimya kikajazwa maana. Msomaji wa drama mwenye tajriba na makini atabuni miondoko yake. Lakini hata msomaji asiye na tajriba ni sharti atambue maelezo mahsusi ya miondoko yaliyotolewa katika maelekezo

ya jukwaa. Wasifu, tabia na saikolojia za wahusika huonekena katika utendaji hivyo basi pawe na ubunifu mkubwa wa miondoko ambayo husaidia kuweka wazi mambo hayo wakati wa utendaji.

(*... Anatikisa Kichwa mara kama anayekubaliana na jambo na mara kama mwenye kukataa...*) (uk.40)

Arege, T. ( 2009)

Hisia za kuchanganyikiwa kwa Sele ikiwa akubali 'plastic surgery' au la zinabainika katika miondoko hii.

(*...Fatuma anatokea kushota na Mambo anatokea kaskazini. Wanakutana.*) (uk.12)

Mbatia, M. (*2006*)

Miondoko hii inabainisha misimamo tofauti ya wahusika.

(*...Anaranda kutoka sehemu moja ya chumba hiki huku akikagua visaraka kadhaa kabla ya kusita. Anashika kiuno kwa mikono yake kama asiyekubaliana na jambo fulani. Anaketi...*) (uk.1)

Arege, T. ( *2011*)

Mwondoko, mwendo au msogeo kama huu wa wahusika huonekana kwa kutazama miili na viungo vya miili vya waigizaji na hutilia mkazo kwenye tukio husika. Miondoko hii ya Daktari Siki yanaonyesha wazi kuwa mambo sio shwari pale zahanatini.

## 2.6 Uangazaji

Mwangaza huiwezesha hadhira kuona vyema waigizaji na matendo yao. Uangazaji huongeza umuhimu katika utendaji na kutuelekeza kwenye athari maalum. Wamitila (2011) ameeleza kuwa uangazaji wa jukwaa ni muhimu katika uigizaji. Taa hutumiwa kulimulika eneo walipo wahusika wanaotenda tendo fulani. Taa hizi huweza kutumiwa kwa namna ambayo inazua picha fulani au halimahasa au mazaji na kulifungamanisha na tendo kuu. Kwa mfano, taa nyekundu kuonyesha hatari, giza kuonyesha uovu au ukosefu wa mwelekeo na taa hafifu kuonyesha kukosa uhakika au msimamo. Uangazaji hivyo basi una uwezo wa kuzua hisia za furaha, masikitiko na hata hasira. Katika kazi ya uigizaji, mazaji hujitokeza vyema jukwaani kuliko katika maandishi.

Griffiths na Hemming ( 1984:112) wanasema kuwa hata ingawa jukwaa halina vifaa au upeo wa athari inayopatikana katika filamu, ni bayana kuwa muziki na uangazaji huzua msisimko, hutoa rangi za kupendeza na matokeo ya kiishara.

Butler (1975:7) anasema kuwa ni muhimu hadhira kuona miondoko na ishara za uso za waigizaji. Hili ndilo kusudi la kwanza la uangazaji wa jukwaa. Pia, mazingira yanaweza kubuniwa kutokana na jinsi mandhari ya jukwaa yameangaziwa. Taa zilizoundwa kwa ustadi na mifumo iliyodhibitiwa hupendeza au huvutia.

Wilson (1998:409) anasema kuwa kama vipengele vingine vya utendaji, uangazaji wa jukwaa una kifanani katika maisha ya kila siku ambapo jukumu la kimsingi la uangazaji kwa kawaida ni kuangaza na kuwawezesha watu kuona usiku na mahali ndani ya

nyumba. Kuna matumizi mengi ya kithieta ya mwangaza katika maisha ya kila siku. Ishara za matangazo kila mara hutumia rangi ya neoni au taa zilizo na rangi zenye kung'aa. Mikahawa huonyesha rangi hafifu na mishumaa. Nyumbani watu huweka mwangaza katika sehemu maalum za vyumba kama vile chumba cha mankuli. Watu pia hutumia vidhibitiumeme ili kuweza kupunguza mwangaza ili kubuni halimahasa. Athari yenye nguvu ya uangazaji wa jukwaa ni kwamba uangazaji ni mojawapo ya rasilimali yenye nguvu inayoonekana katika thieta na inayoweza kutumika kwa njia mbalimbali: Walakini kuna wakati mwangaza hufifia. Ufifiaji huu hudhamiriwa kuchochea au pia kuzima taharuki kwa hadhira kutegemea mchezo.

Wilson (1998:411) amewataja wasanii na wapangaji wa mandhari wenye ubunifu. Kuhusu madhumuni na majukumu ya uangazaji, amemtaja Adolphe Appia aliyeishi kati ya mwaka wa 1862- 1926, mswisi, msanii mwenye ujuzi katika kubuni mandhari kuwa miongoni mwa wale wasanii wa kwanza kuona umbuji mkubwa sana au uwezekano wa usanii wa uangazaji katika thieta na kutambua kuwa mwangaza ni elementi muhimu katika utendaji. Pia amemtaja mfuasi wa Appia, Geddes, Mwamerika mwenye ubunifu aliyeishi kati ya mwaka wa 1893-1958 aliyesema kuwa uangazaji mzuri huongeza mwanda, kina, halimahasa, fumbo, mwigo wa kubeza, kinyume, mabadiliko ya hisia, mahusiano na hofu. Naye Edward Gordon Graig, Mwingereza mvumbuzi aliyeishi kati ya 1872- 1966 akatajwa kama msanii aliyezungumza kuhusu kupanga rangi kwa kutumia mwangaza.

Uangazaji katika jukwaa hutuwezesha kuona, hufichua maumbo husaidia katika kubuni halimahasa na pia husaidia kubuni muda na mwanda. Huimarisha yale yanayoonekana kwa kuelekeza hadhira kwenye tukio linaloendelea katika sehemu fulani ya jukwaa.

Haya yanaonekana katika mifano hii:

> *Onyesho hili lina mwangaza mchache… spotlaiti inatulia*
>
> *kwa muda mrefu juu ya kichwa cha Kitaru….(*uk. 30)
>
> (*Spotlaiti meza ya kwanza*) (uk. 42)
>
> Hussein, E. (*1971*)

**2.7 Sauti**

Sauti ni kipengele cha utendaji ambacho hakionekani kama vipengele vingine lakini husikika. Siku za hivi karibuni sauti imekuwa kipengele muhimu cha kithieta kutokana na ubunifu wa kithieta, usanii, teknolojia na usanifu wa kipekee. Njia moja ya kuainisha usanii wa sauti ni kwa sauti iliyobuniwa upya na sauti iliyoimarishwa kulingana na maoni ya Wilson (1998:423). Kubuniwa upya kulingana na mwandishi huyu ni sauti kutokana na motisha au sauti za kimazingira. Sauti kutokana na motisha huweza kuwa kama vile magurudumu ya gari yakichuana na changarawe, gari likigeuzwa au mlango ukigongwa ambao unaweza kutangaza kuingia kwa mhusika katika sehemu ambayo tendo linatokea. Hizi ni sauti ambazo hudaiwa na matini. Sauti za kimazingira ni zile za kutoka katika maisha ya kila siku ambazo husaidia kubuni kinachoelekeza ukweli au kinachoaminika. Katika utunzi, sauti za magari mjini, sauti za chenene mashambani na sauti kubwa ya muziki wa roki katika bweni ni sauti ambazo husikika kichinichini. Kiwango kizuri cha muziki uliyoteuliwa kwa makini na athari ya sauti ni viungo muhimu

vya thieta. Kuna sauti zinazotolewa na waigizaji na zinazosikika nyuma au nje ya jukwaa.

Kwa mfano:

(… *saa ya ukuta inasikia ikilia tik tak… tik tak…*) ( uk.83)

Arege (2009)

(.. *Mara rukono yake inalia…*) (uk.1)

(… *kuna milio ya watoto inayosikika…*) (uk.34)

Arege ( *2011*)

Sauti hizi katika tamthilia hizi zinaonyesha hali ya wasiwasi na pia kudhihirisha kuwa mambo si shwari. Mlio wa saa unaosikika nyumbani kwa Sele ni ishara kuwa muda unaendelea kuyoyoma bila ya tiba ya Sele kupatikana. Milio ya simu na ya watoto katika zahanati inabainisha kuwa wagonjwa wanaendelea kuteseka zahanatini huku Daktari Siki akionyesha kushindwa na la kufanya.

**2.8 Kimya**

Griffiths na Hemming (1984:116) wanasema kuwa uzingativu wa hadhira unavutiwa zaidi na maneno au miondoko. Mhusika anayezungumza huenda akashughulisha macho na masikio. Ikiwa mhusika bubu aliye kimya ataingia au atatenda mwondoko wazi, yeye atavuta mawazo. Kimya kinaweza kuwa na umuhimu sana. Wakati wa kusoma tamthilia kila mara husaidia katika kukumbuka nani yuko katika jukwaa na hazungumzi.

Wamitila (2002:90) katika kushughulikia kimya na mtuo katika uhakiki wa tamthilia anasema kuwa tuisomapo tamthilia hatuwezi kuutambua uzito wa kisanaa pamoja na athari inayotolewa na matumizi ya kimya au mtuo. Mtuo unaweza kutumiwa kusisitiza kauli fulani na kuifanya hadhira kuiwazia. Pia hutumiwa kuikuza hali ya hisia kwenye usimulizi na uigizaji. Kimya huweza kutumiwa kusisitiza kiwango cha athari ya kisanaa na maneno fulani. Pia husisitiza na kuchimuza au kulifanya jambo maalumu litokeze mbele ya mengine na kuweza kuwazia kwa makini.

Kwa mfano:

(*Kimya kirefu* ) (uk.25)

Hussein (1969)

Kimya hiki kinatoa nafasi ya kuwazia msukumo na hamu ya mhusika Kitunda katika vita.

**2.9 Mihimili**

Kwa maoni ya Griffiths na Hemming (1984), mihimili huchangia ufahamu wa yanayoonekana. Vifaa vyenye maumbo yanayoonekana ni muhimu sana hasa katika utani au mchezo wa kuchekesha. Huweza kudhihirisha tendo, huweka wazi tabia au kuashiria dhamira au wazo. Kwa mfano chupa na bilauri za vileo ni mihimili ambayo aghalabu hutumika kudokeza starehe. Hivyo basi vitu hivi vya ziada vinasaidia kuipa tamthilia mvuto wa kisanaa

Kwa Mfano:

(*...ameshika kizinga cha moto ...*) (uk.4)

Hussein ( 1969)

Mhimili huu unadhihirisha kuwa matukio yanafanyika wakati wa usiku na pia kubainisha hali ya ukosefu wa maendeleo ya kiteknolojia na kiuchumi ambapo kizinga kinatumika badala ya kurunzi.

## 2.10 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia ufafanuzi wa vipengele vinavyofanikisha utendaji ambavyo ni: maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili. Katika sura inayofuata tumevitathmini vipengele vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya.*

# SURA YA TATU

## 3.0 Vipengele vya Utendaji Katika Tamthilia ya Kimya Kimya Kimya

Katika sura hii ya tatu tumetathmini matumizi ya vipengele vinavyofanikisha utendaji katika tamthilia ya K*imya Kimya Kimya. Kimya Kimya Kimya* ni tamthilia inayohusu mvutano baina ya wahusika Kulia na Kushoto ambao umekuwa mzito. Mbele hawaendi, nyuma hawaendi, kulia na kushoto hawaendi. Kushoto anataka kwenda kulia hawezi, Kulia anataka kwenda kushoto naye hawezi pia. Kwa kuelekezana migongo na kuvutana pande zote hawaendi popote. Kumbe sababu ya haya yote ni kimya. Hali hii itabadilika pale tu watakapokaa kimya na wakiruhusu kimya kusema. Inakuwa vigumu kila mara wananchi kushindwa kukabiliana na matatizo yanayowakabili kwa sababu ya kuwa na misimamo tofauti na kukosa kushirikiana.

## 3.1 Maelekezo ya Jukwaa

Maelekezo ya jukwaa ndiyo msingi wa yale yote yanayotendeka kwenye jukwaa. Hii ni kwa sababu vipengele vingine vyote vya utendaji hubebwa na maelekezo haya. Hivyo basi, kipengele hiki ndicho kitovu cha vipengele vya utendaji katika tamthilia. Katika kuangazia maelekezo ya jukwaa katika K*imya Kimya Kimya*, utafiti wetu unatathmini ikiwa Mohamed amefanikiwa katika kukitumia kipengele hiki kama msingi wa vipengele vya uigizaji ili kuiwezesha kazi yake kuigizika kwenye jukwaa. La muhimu kwetu ni kuchanganua ikiwa katika maelekezo ya jukwaa mtunzi huyu amedokeza mandhari, maleba, uangazaji, miondoko, sauti, mihimili na kimya. Tunatathmini ikiwa maelekezo haya yanaweza kutegemewa na waigizaji wanaouwasilisha ujumbe wa tamthilia hii katika jukwaa.

### 3.1.1 Mandhari

Mandhari ni kipengele kinachofanikisha uigizaji wa ujumbe kwenye jukwaa. Sehemu hii inatathmini ufanisi wa Mohamed katika kukitumia kipengele hiki katika kazi yake ili kufanikisha uigizaji wa tamthilia yake kwenye jukwaa.

**Kifunguzi**

> *Wapotea njia...Mmoja anatokea kushoto ya msitu, anaitwa Kushoto. Mwingine anatokea kulia ya msitu, anaitwa Kulia...Wanakutana kwenye kisima. Kisima kikavu cha maji yasiotekeka.* (uk.8)

Katika onyesho la pili:

> *(Pale pale kisimani...)* (uk. 19)
>
> *(... polepole anakinyemelea kisima. Afikapo karibu na kisima anaigeukia hadhira.)* (uk. 20).
>
> *(Mpya anaelekea kwenye kisima polepole, kimya kimya, hatua kwa hatua. Pale kisimani anasita).* (uk. 22)

Maelekezo haya yanafichua mahali pa utendaji. Ni katika kisima hiki ambapo wahusika Kulia na Kushoto wanapokutana wakiwa na njaa na kiu lakini wanatamaushwa na ukavu wa kisima hiki. Itawabidi kuiacha misimamo yao tofauti, washirikiane na waseme ili waweze kutatua shida zao. Mhusika Mpya pia anaelekezwa kwenye kisima hiki ambacho sasa kinabadilika na kuwa amali muhimu ya jamii ambapo suluhu itapatikana. Hapa ndipo Mpya atatunukiwa ujasiri wa kusema ukweli bila hofu.

Katika onyesho la pili:

> (… *Familia ya Mzee Binafsi iko mezani. Mpya, mdogo wao wa miaka ishirini na moja hivi kaketi upande mmoja peke yake. … Mussa na Zanga upande mwingine wa meza. Bi. Shoo (Mama mtu) yuko kwenye ncha moja ya meza. Katika ncha nyingine ya meza kuna kiti ambacho mpaka sasa kitupu).* (uk. 27)
>
> (… *Familia ipo mezani inangojea chai inywiwe…*) (uk. 29)
>
> (…*Watumishi wanamsindikiza mpaka kwenye kiti chake cha enzi* …) (uk .33)

Maelekezo haya yanawabainishia waigizaji kuwa sehemu ya tendo ni mezani ukumbini kwa Mzee Binafsi. Maelekezo haya pia yanabainisha wakati. Ni asubuhi kwani vyakula vya kila aina vinawangojea kufungua vinywa. Mhusika mpya anaonekana kutengwa na wengine. Pale mezani sehemu maalum anapoketi Mzee Binafsi inaangaziwa. Bwana Binafsi anaubeba ukuu wake hadi nyumbani kwake. Wasifu wake unabainika kama mtu mwenye majivuno na ambaye si kielelezo cha mzazi mzuri kwani ameitusi asasi ya jamii.

Katika onyesho la tatu:

> (… *Chumbani mwa vijana wawili wa kiume – Mussa na Zanga. Chumba cha kitajiri. Chumba chenye vitanda vya kisasa. Kimoja cha Mussa – sasa kitupu – chengine kimelaliwa na Zanga. Samani na mapambo yaliyomo chumbani pia ni ya kisasa na kitajiri. Usiku wa manane.* (uk. 45*).*

Maelekezo haya yanaaangazia mahali pa uigizaji. Ni nyumbani kwa Bw. Binafsi. Hii ni nyumba ya kifahari. Mali hii imelimbikizwa kutokana na matumizi mabaya ya mali ya umma. Vile vile yanabainisha kuwa ni wakati wa usiku.

(... *Inazuka na kuenea chumbani mwa akina Mussa na Zanga.*) (uk. 49)

Maelekezo haya yanasisitiza mandhari yale ya chumba cha Mussa na Zanga ambapo sauti ya Mpya inasikika kama mwangwi ikiwasihi watu washirikiane kutetea haki.

(*Bustani ya taifa jijini...*) (uk. 57).

(...*Askari wanamiminika na kuingia bustanini...*) (uk. 61).

Mazingira yamebadilika kutoka nyumbani kwa Bwana Binafsi hadi bustani ya taifa, mahali ambapo wananchi wanakusanyika kwa mkutano wa dharura lakini idadi kubwa ya askari wanawatawanya kwa virungu. Hii ndiyo njia inayotumiwa na Bw. Binafsi kuwakandamiza wapinzani wake ili kuhifadhi cheo.

Katika onyesho la tano:

*Ofisi ya kiongozi mkuu yaani Bw. Binafsi. Yeye mwenyewe ameketi kwenye kiti maalum... kulia ya mkuu anaketi waziri wa nchi Bw. Naona, na kushoto anakaa ofisa wa usalama Bw. Salimina. Pana vinywaji vya kila aina.* ...(uk. 63)

*Bw. Binafsi ameingia kwa pupa ofisini mwake...* (uk.77)

Mandhari haya yanabainisha ukuu wa Bw. Binafsi pamoja na wanaomzunguka. Vinywaji vya kila aina ni taswira ya starehe lakini hakuna nafasi ya kuvinywa kutokana na malalamiko ya wananchi. Pia katika onyesho la saba, Bw.Binafsi anaonekana amejawa na hisia za mchanganyiko anapoingia ofisini kwa pupa. Bwana huyu ana hasira, hofu na

wasiwasi kwa sababu cheo chake kimo hatarini. Juhudi zake za kunyamazisha umma zimegonga mwamba huku waasisi wa maasi dhidi yake wakiwa wanawe ambao hawapatikani kwa sababu wamefichwa na kuhifadhiwa na umma.

Katika onyesho la sita:

*Watu wachache wanatembea njiani* ... ( uk. 72)

Hapa waigizaji wanaelekezwa katika mazingira ya njiani ambapo wananchi wanasikiza sauti ya Mpya ambayo imeenea nchi nzima na wako tayari kushirikiana naye katika harakati za ukombozi.

Katika onyesho la nane:

(... *Bw. Binafsi na Bi. Shoo wamebwatika juu ya sofa kwenye ukumbi wao wa fahari.*) (uk. 84)

(... *wananchi wamelizunguka kasiri lao.* ) (uk. 87)

Mandhari haya ya jukwaa yanarejea katika nyumba ya Bw. Binafsi. Kubainisha hali ilivyo baada ya maasi ya wananchi wakiongozwa na wana wa Binafsi. Starehe katika kasri hili si starehe tena kwani kelele za wananchi zimezidi na wako tayari kumng'oa kiongozi huyu mamlakani.

Mwandishi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, Mohamed (2011) amebainisha ubunifu mkubwa katika kutumia kipengele cha mandhari. Ametumia mandhari halisi kama vile msitu, kisimani, nyumbani kwa Bw. Binafsi, bustani ya taifa jijini, njiani na ofisini. Mandhari haya yanawaelekeza waigizaji katika mazingira ya utendaji katika jukwaa. Mandhari yanabadilika kulingana na majukumu. Wakati mwingine anarejelea mandhari

yale yale inapohitajika. Mandhari yamekuwa na athari kubwa katika kuwasilisha ujumbe wa mwandishi.

### 3.1.2 Maleba

Kipengele hiki huchangia pakubwa katika kufanikisha uigizaji wa tamthilia kwenye jukwaa. Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele hiki katika tamthilia *Kimya Kimya Kimya.*

Katika onyesho la pili:

> (*... ameota upara katikati ya kichwa , nywele zimefinga mvi zote....*) (uk. 33)

Maelekezo haya yanawawezesha waigizaji kumuiga Bw. Binafsi anavyoonekana. Nywele ni kifuasi cha maleba. Hapa nywele zimebainisha hali halisi ya Bw. Binafsi. Yeye ni mzee anayetarajiwa kuongoza kwa hekima lakini mambo ni kinyume kwa sababu hana sera zozote za maendeleo.

Imebainika kuwa hiki ni kipengele adimu katika tamthilia hii. Umri wa mhusika Bw. Binafsi unadokezwa kwa kupitia nywele ambazo ni kifuasi cha maleba. Waigizaji wameachiwa jukumu la kubuni maleba kuambatana na ujumbe. Kwa mfano familia ya Bw. Binafsi inatarajiwa kuwa imevalia mavazi ya kifahari na kisasa ilhali wananchi wanatarajiwa kuwa wamevalia mavazi ya kubainisha umaskini uliosababishwa na uongozi mbaya. Mavazi waliovalia waigizaji pia yana jukumu la kuonyesha wahusika wa kike na wa kiume, askari na wananchi wa kawaida.

### 3.1.3 Miondoko

Sehemu hii inachunguza matumizi ya kipengele hiki cha utendaji katika tamthilia hii ya Mohamed.

katika kifunguzi:

*Mmoja anatokea kushoto… Mwingine anatokea kulia…*

*Wote wana jitimai na hofu ya kupotea….* (uk. 8)

Wahusika Kushoto na Kulia wanatokea pande tofauti za msitu na hatimaye kukutana kwenye kisima. Hisia za nyuso zao zinabainisha hali ya kuwa na huzuni na hofu ya kupotea. Wana njaa na kiu ilihali kisima walichokifikia ni kikavu. Wao ni kielelezo cha wananchi walio na misimamo tofauti.

(*Kushoto anashangaa… Anatoa macho, lakini mara anatabasamu.*) (uk.8)

(*Anakisogelea kisima na kuchungulia ndani. Kisha anaigeukia hadhira.*) (uk. 9)

(*Anaondoka pale alipokuwa kainama kuchungulia kisima na kuisogelea hadhira*). (uk..9)

(*Akiwa bado anachungulia kisimani, anainuka. Anamwona Kulia. Anajificha kichakani.*) (uk.10.)

Miondoko hii inatekelezwa na mhusika Kushoto ambaye anatamauka na kushangaa baada ya kukiona kisima kikavu na kinachosema. Sauti kutoka kisima inamhimiza aijali nchi inayohitaji mchango wake ili kuwe na mabadiliko.

(*Anaingia Kulia. Anatokeza kichakani na kuelekea kisimani.*)

(uk.10)

(*Kulia anasita na kutazama huku na huku kwa mshangao,*

*kisha …*) ( uk.12)

Mhusika Kulia pia akiwa na wasiwasi anashangazwa na kisima hiki ambacho zamani kilibubujika maji lakini sasa mna ombwe. Hiki ni kielelezo cha hali ilivyokuwa kabla ya nchi hii kuongozwa na kiongozi asiyekuwa na sera za maendeleo. Yeye pia anahimizwa na kisima hiki asiangalie nyuma bali aijali nchi. Wawili hawa wanajisaka na wanajaribu kuelewana. Ni sharti wahimizane kuzika tofauti zao ili waweze kushirikiana kuiokoa nchi kutokana na uongozi mbaya.

(*Sasa Kulia ananyanyuka kutoka pale kisimani*) (uk.13)

*(Anatoka kisimani na kumsogelea Kulia.* ) (uk.13)

(*Wanasogeleana. Wanasita wanapokaribiana pua na*

*mdomo. Wanaanza kutazamana jicho kwa jicho…*) (uk. 14)

*(Kushoto anageuka kuelekea kulia na Kulia anageuka*

*kuelekea kushoto… wanagusana mgongo kwa mgongo….*)

(uk. 15)

*(Wanasukumana. Kushoto anamsukuma Kulia arudi*

*kulia na Kulia anamsukuma Kushoto arudi kushoto.* )

(uk.15).

Katika onyesho la kwanza:

(*Anacheka... wanasukumana kimgongomgongo ...*) (uk.17)

Mhusika Kulia anachoshwa na hali hii ya mvutano. Miondoko hii inayotekelezwa na Kulia na Kushoto inadhihirisha hali ya mvutano kutokana na misimamo yao tofauti na athari zake kwani haiwapeleki popote. Wamekwama hata baada ya kubadilishana pande walizotoka. Wawili hawa wako katika harakati za kujaribu kufahamiana. Kuna nguvu fulani zinazowazuia kurudi walikotoka na kutengana tena.

(... *Anawapita Kulia na Kushoto...*) (uk. 19)

*(Anaiendea hadhira na kuitumbulia macho yaliyojaa bumbuazi... kisha anatazama kwa hofu – kulia, kushoto, nyuma na mbele., kama vile anaogopa kuonekana na mtu... Baadaye anatazama juu huku pole pole akinyemelea kisima. Afikapo karibu na kisima anaigeukia hadhira. Anasema nayo kwa kumungunya midomo... Anatazama tena huku na huku... Anaijongelea hadhira mpaka anakuwa karibu kuyeyuka nayo.* ) (uk. 20).

*(Anawageukia Kulia na Kushoto na kushangaa jinsi walivyoambatana na kusuguana migongo*) (uk. 21)

*Anaonyesha kidole kwa akina Kulia na Kushoto.* ) (uk. 22)

Mhusika Mpya anaonekana kuhofishwa na hali ya Kulia na Kushoto ya kutoshirikiana anawanyoshea kidole ili kuwatahadharisha kuwa utengano ni udhaifu. Anasema kwa kumumunya mdomo bila kutoa sauti ili kuonyesha hofu, wasiwasi na tahadhari ya kusikika kwani hakuna anayeruhusiwa kusema kwa sauti katika nchi hii. Anaikaribia hadhira ili aweze kutangamana nayo na ili ipate kumsikia.

> *Mpya anaelekea kwenye kisima polepole … hatua kwa hatua … kisha anageuka kutazama huku na huku. Kushoto na kulia, nyuma na mbele, juu na chini. Halafu anakigeukia kisima …Kisha ghafla anatumbukia kisimani… Mpya anaibuka kisimani… Taratibu anaibuka huku kanyanyua mikono inayonyanyua bakuli la maji juu…)*
>
> (uk. 23)
>
> (*… Mpya anapeleka kiamo kinywani nakugugumia maji ya ujasiri kisha anajimwagia majiyaliyobaki mwilini mwake. Kulia na Kushoto wanabagukana na kugeukiana na kutazamana kwa uso.*) (uk. 23)

Maelekezo haya ni marefu kutegemea jukumu lake katika uigizaji. Mhusika Mpya anaelekea kwenye kisima polepole na kugeuka huku na huku ili kuonyesha wasiwasi na tahadhari. Anaelekea kutenda jambo lenye umuhimu mkubwa. Hili ni tambiko la uhai. Ni tambiko la kusema ukweli bila kuhofu wala kuogopa. Tambiko la kumwezesha kujitolea mhanga. Kutokana na tambiko hili Kulia na Kushoto wamefahamiana.

Katika onyesho la pili:

(*Wote walio jukwaani wanaziba masikio. Wote wanashangaa, lakini Mama nyumba anajaa hofu kuliko wote.*) (uk. 27)

Familia ya Bw. Binafsi inatumia mikono yao kuziba masikio. Nyuso zao zinaonyesha mshangao na hofu. Wanafanya hivyo kutokana na mpasuko mkali wa chuma kuanguka sakafuni. Hakuna anayeruhusiwa kusema au kutoa sauti katika nyumba hii na hata katika nchi hii.

(*… Wote wanavikodolea macho vyakula kwa matamanio*) (uk. 29.)

( *… Hapo kitini alipoketi Mpya anaonekana ana huzuni nyingi… Watu wote katika familia wanalambatia mate…. Yeye anatazama hewani … hatimaye memba wa familia yake waliokaa vitini wanampa ishara ya kumgombeza asitazame juu…*) (uk. 30)

Maelekezo haya yanamtofautisha mhusika Mpya na familia yake. Nyuso zao zinaonyesha tamaa ya vyakula ilhali uso wake unaonyesha huzuni. Yeye analambatia haki ya kusema.

(*Anaigeukia hadhira …*) ( uk. 31)

(*Sasa anamtazama kila mtu aliyekaa hapo kwa jicho la dharau na kulaumu.*) (uk. 31)

Macho ya mhusika Mpya yanadhihirisha hisia za dharau na lawama kwa familia yake ambayo imesalimu amri ya Bw. Binafsi. Anawalaumu kwa sababu ya kuogopa huku

wakifahamu vizuri kwamba wanadhulumiwa kwa kunyimwa haki ya kusema. Mpya anaigeukia hadhira ili aseme nayo kwa sababu amechoka kusubiri.

> (*Anasimama na kuonekana anataka kusema kitu, lakini anasita na kubakia kumtazama Mpya kwa jicho kali la hasira… Anatabasamu tu … Bi Shoo hatimaye anaketi … Anaingia Bw. Binafsi kwa matao. Akiongozwa na walinzi wake wawili. Anaingia ukumbini kwa madaha na watumishi wanamsindikiza mpaka kwenye kiti chake cha enzi… Mtumishi mmoja anamvutia kiti, anapita na mtumishi mwingine anakiingiza taratibu kiti ndani chini ya meza. Huku Bw. Binafsi anaketi… Anamkagua mtu mmoja mmoja hapo mezani. Wote wanainamisha kichwa chini, isipokuwa Mpya ambaye yeye amemtumbulia macho namna ile ile baba amemtumbulia yeye.*) (uk. 33)

Maelekezo haya yanadhihirisha hofu aliyo nayo Bi. Shoo kuhusu kuvunjika kwa nyumba yake. Hisia za ukali na hasira zinaonekana katika macho yake anapomtazama Mpya. Uhusiano mbaya kati ya Bw. Binafsi na familia yake unaonekana. Bw. Binafsi ni mtu mwenye majivuno na kiburi anaingia kwa maringo ilhali familia yake imemsubiri kwa muda mrefu. Ujasiri wa Mpya pia unaonekana anapomtumbulia babake macho.

> (*Anamtolea kidole cha shahada.*) (uk. 34)
>
> (*Anamtazama kila mtu … Anatabasamu …*) ( uk. 35)
>
> (*Wote wanakula kwa pupa na hamu… baadaye Binafsi anainua uso na kumwona hali …*) ( uk. 35)

(... *Akitabasamu na kufungua dimba*) (uk. 36)

Bi.Shoo: *(Huku, akitabasamu na kujitia ucheshi mwingi.)* ( uk. 36)

Bw. Binafsi: *(Anaonekana amefurahi.*) ( uk. 37)

Mussa: *(Ana wasiwasi kidogo.*) ( uk. 37)

Zanga: *(Wasiwasi wake unazidi mwisho wa maneno yake.*) ( uk. 38)

Bw. Binafsi: *(Anasita na kumtupia jicho Mpya ...* ) ( uk. 38)

Bi. Shoo: (*Kwa hofu heshima na taadhima.*) ( uk 39.)

Miondoko hii inayotendeka pale mezani inasaidia kujenga ukamilifu wa kimaana na kisanaa. Mpya anaonywa kwa kidole kwa sababu kila mtu pale mezani ameinamisha kichwa kama ishara ya heshima na utiifu ilhali yeye amemtumbulia macho babake. Bw. Binafsi anaonekana kuridhika na utiifu wa bandia wa mkewe na watoto wake wa kiume Zanga na Mussa wanaoungama utiifu kwa zamu. Wanafanya hivyo huku wakila matonge makubwa kuonyesha hamu na pupa kwani wamesubiri kwa muda mrefu kwa sababu hakuna anayeruhusiwa kula kabla ya Bw. Binafsi kuingia. Mpya hatarajiwi na babake kuungama utiifu. Bw. Binafsi anamdunisha mkewe mbele ya wanawe kwa kumtusi baada ya kusikia sauti nyuma ya jukwaa. Hachukui muda kuthibitisha asili ya sauti. Anapapia mambo kudhihirisha ukosefu wa hekima.

(*Akimgeukia Bi. Shoo.* ) ( uk. 40)

(*...Lakini Mpya anaonekana kasawijika. Ana huzuni nyingi.*)

( uk. 40)

(*Anamwonyesha Mpya kidole.*) (uk. 40)

*(... Wote wanashangaa na kunyong'onyea.... Anasimama na kuchopoka kitini kwa ghafla na kuwaamrisha walinzi wake kumwendea Mpya. Walinzi wanamshika mkono na kumburura kama gunia la makaa.*) (uk 41)

*(Bi. Shoo anaenda na kumshika mkono Mpya na kuanza kutoka naye taratibu kwa huzuni nyingi. Kuona hivyo, wale wote walioko mezani wanasimama na kumfuata mama yao...*)

( uk. 42)

Bw. Binafsi ni kielelezo cha kiongozi duni ndani na nje na amejiwekea ulinzi mkali na kuwakandamiza wale wanaomkosoa. Anataka kusema na mkewe ana kwa ana ili aweze kuona hisia zake kuhusu binti yao. Mpya anahuzunishwa na babake ambaye badala ya kuuona na kukubali ukweli wa mambo anamkana mwanawe eti kwa kumpaka kinyesi. Familia ya Bw. Binafsi inashangaa na kuhuzunika kwa sababu ya udhalimu wa Bw. Binafsi. Wameonyesha wazi kuwa wamechoka na wako tayari kumuunga mkono Mpya.

( *... Bw. Binafsi anageuka na kuelekea jikoni au upande unaotokea mpasuko wa sauti.)* (uk. 43).

Sauti sasa inasikika kote na hii ni ishara ya maasi dhidi ya Bw. Binafsi. Vitu vingi vimeanza kusema na kumkashifu Bw. Binafsi.

( *Anaweka kidole chake cha shahada cha mkono wa kulia*

*juu ya mto… Anasongea kwenda kumfungulia dirisha Mussa. Mussa anaingia ndani kwa kutumbukia dirishani…)* (uk. 45)

*(Anasita. Anaonekana ana wasiwasi mwingi.* ) (uk. 48)

Mto na kidole mdomoni ni kwa sababu ya kuzuia sauti isisikike kwa sababu vijana hawa hawana uhuru wa kusema. Mussa anakiuka amri ya babake na kutoka nje usiku. Anamwambia kakake Zanga kuwa amechoka kuongozwa na mawazo ya mtu mwingine kama kinyago. Ujasiri wa Mussa katika kutafuta haki na uhuru wa kutenda na kusema unabainika. Jambo hili linamshangaza kaka yake Zanga ambaye bado anaogopa. Wasiwasi wa Zanga unatokana na yeye kutoelewa maneno ya Mussa anayesema kuwa upande mmoja wa giza hutisha na upande mwingine huhifadhi. Anasema maneno haya ni magumu, fichizi na tatanishi.

Katika onyesho la nne:

*…Wanaingia mmoja mmoja, wawili wawili na hata vikundi vikundi.* (uk. 57)

(*Anaingia Bw. Taja.*) (uk. 57)

(*Anainuka pale penye kiburunji alipoketi na wenzake na kumlaki rafikiye Bw.Taja.*) (uk. 57)

(*… Anaingia bila ya kuwaamkia watu)* (uk. 57)

*(Ghafla linaingia kundi la wananchi wakiongozwa na Mpya na kaka zake. Watu wote waliopo wanasimama na kusherehekea…*) (uk. 61.)

(*… Askari wanamiminika na kuingia bustanini na virungu*

*vyao. Vurugu linaanza. Wananchi wanapigwa virungu.*

*Wananchi wanakimbia huku wakilalamika*) ( uk. 61)

Maelekezo haya yanawasaidia waigizaji kuigiza pingamizi na dhuluma za Bw. Binafsi katika jaribio lake la kunyamazisha umma. Wananchi wamekusanyika kwa mkutano wakiwa na hamu ya kusema na wana wa Bw. Binafsi. Sauti ya Mpya imesikika kote. Mkusanyiko huu unatawanywa na Askari wengi kwa kutumia virungu vyao. Hii ndiyo mbinu inayotumiwa na kiongozi asiyekuwa na kipawa cha kuongoza ili kuhifadhi cheo .

Katika onyesho la tano:

***Wasiwasi wa wazee!*** (uk.62)

Maelezo haya yaliyo katika wino uliokolezwa yanaonyesha kung'amua kwa viongozi kuwa wamo mashakani kwani wananchi wameamua kusema bila kukoma na bila hofu.

(*... waziri wa nchi na ofisa wa usalama wanaingia ofisini na kutoa saluti.*) (uk. 63)

*(Sasa waziwazi amekasirika.*) (uk. 64*)*

(*... Mheshimiwa kiongozi mkuu, anachezesha kalamu mkononi...*) (uk. 65)

(*Kwa hasira kubwa zaidi...*) (uk. 67)

(*Kwa ukali.*) (uk.67)

Bw. Binafsi ana hamaki baada ya kuelezwa kuwa watu wanadai uhuru wa kusema na pia wataka katiba ya nchi ibadilishwe. Saluti ni ishara ya heshima. Linalomkera zaidi ni kuambiwa ukweli kwamba maasi haya yalianzishwa na wanawe.

Katika onyesho la sita:

*Watu wachache wanatembea njiani. Wanapita na kupituka.*

*Wanapita huku na kurejea huko…*) (uk. 72)

*Bw. Binafsi anaingia kwa pupa ofisini mwake …*

*Anatumbulia macho ile meza. Halafu anageuka nyuma*

*kuitazama hadhira… Kisha anapiga hatua … kisha*

*anageuka kulia. Anapiga hatua za masafa kama mwanajeshi.*

*Sasa anafululiza kutembea huku na huku kama askari*

*mlinda doria.*) (uk. 77)

Miondoko hii ya uradidi inaonyesha hasira, wasiwasi, hofu na ukosefu wa raha kwa Bw. .Binafsi. Wanawe ambao sasa anawarejelea kama mafisadi hawapatikani na huku umma unaendelea kulalamika na kukosa utulivu. Bw. Naona na Bw. Salimina wanafukuzwa kutoka ofisini hata baada ya kuonyesha heshima kwani wameshindwa kumhifadhi Bw. Binafsi cheoni kwa kuwanyamazisha watu..

(*Anaigeukia hadhira ghafla.*) ( uk. 77)

*(Sasa anageuka na kuelekea kwenye meza yake. Anaketi*

*hapo. Lakini ghafla anasimama anapomwona seketari wake…*)

(uk. 78)

(… *Anaanza kuzungumza kuzunguka huku na huku* …)

(uk. 78)

(… *Bw. Naona na Bw. Salimina wainuka na kotoa saluti*

*halafu wanatoka.*) ( uk. 80)

(… *Analiendea lile yoo….*) (uk. 80)

(*Akionekana ana huzuni nyingi kabisa…*) (uk.81)

( *Bw. Binafsi anaanguka chini.*) (uk. 82)

Yoo linamchorea Bw. Binafsi picha ya matukio katika uongozi wake kwa kuakisi maovu yote aliyotenda akiwa uongozini. Bw. Binafsi anazungumza na nafsi yake kupitia hili yoo. Upande mmoja unamsihi ajiuzulu huku upande wa pili ukimhadaa kuwa uongozi huo ni wake pekee. Hii ndiyo hali ya Bw. Binafsi na mkewe baada ya kusikia sauti za wananchi waliokasirika.

Katika onyesho la nane:

> ... *Nyuso zao zimesawijika kwa jitimai na hofu (* uk. 84)
> (*Kundi la watu wanaobeba mabango mbele ya hadhira linapita....*) (uk. 84)
> (*Anamgeukia mumewe.*) (uk 84)
> (*Anaruka hapo alipoketi kama mkizi na kutua mbele ya hadhira.*) (uk. 84)
> (*Anamtolea kidole.*) (uk. 8)
> *(Naye anaruka kuliko mumewe na kutua ubavuni pake .)* (uk. 85)
> (*Anapita huku na huku kainamisha kichwa na huku mikono kaifunga nyuma ya mgongo.* ) (uk. 85)
> *(Anasita kidogo, halafu anaendelea na mchezo wake wa kwenda nyuma na mbele.* ) ( uk.85)
> (*Na yeye naye anafanya kwenda nyuma na mbele lakini anarusharusha mikono*) (uk. 86)

Maelekezo haya yanaonyesha hali ya Bw. Binafsi kutokana na hofu ya kupoteza ukuu wake. Umma sasa unasema naye waziwazi kupitia mabango. Vitimbi kati yake na mkewe vinaonyesha jinsi wanavyoelekezeana kidole cha lawama kwa kukosa la kufanya ili kujiepusha na yaliowapata. Uso wa Bi. Shoo unaonyesha hasira na hofu. Anamuiga mumewe huku akirusharusha mikono kuonyesha kero.

(... *Wote wawili wanashtuka na kuonekana wakisikiliza sauti za wananchi kwa makini...*) (uk. 87)

*(Anaanza kushuka matao ya chini. Anajongea kwenye hadhira. Anaonekana kakata tamaa na huzuni nyingi zimemvaa.*) (uk. 87)

Bw. Binafsi amegundua kuwa mwisho wake umefika. Anaamua kujiuzulu. Ameshindwa kukabiliana na umma kwani sauti zao zina nguvu kama dhoruba.

Mtunzi wa tamthilia hii ameitumia stadi ya miondoko kwa upana na kwa njia ambayo imefanikisha uigizaji. Amebainisha miondoko ya mwili na viungo vyote vya mwili vikitumika kubainisha hisia na mazaji mbalimbali. Wahusika wake wanasonga kwa ustadi hadi maneno yanayosemwa au kimya kustawishwa na kujazwa maana. Maelezo kuhusu miondoko yanawazesha waigizaji kuionyesha hadhira matendo ya wahusika.

### 3.1.4 Uangazaji

Matumizi ya kipengele hiki pia yamechunguzwa katika tamthilia ya K*imya Kimya Kimya.*

**Giza** (uk. 17)

Giza hili linatokea mwisho wa kifunguzi baada ya wahusika Kushoto na Kulia kugandamana huku wakisukumana kimgongomgongo. Hali hii inaonyesha kukwama na kukosa mwelekeo na matumaini kutokana na misimamo tofauti ya hawa wawili.

... *Mwangaza hafifu... Taratibu nuru inakuwa kali Mpya anapoingia...* (uk. 19)

Ufifiaji wa mwangaza pale kisimani unanuia kuonyesha kukosa uhakika na matumaini na pia kuchochea taharuki. Mpya anapoingia nuru inakuwa kali ili hadhira iweze kuona miondoko yake. Mhusika huyu ni ishara ya nuru kwenye giza na amesimamia ukweli na haki. Amebeba matumaini ya kuwakwamua wahusika Kushoto na Kulia ili wabandukane. Katika onyesho la kwanza:

*(Taa zinazimika polepole ..., mpaka giza linapowafunikia.)*

(uk. 24)

*Giza totoro na totoro ya giza* ( uk.25)

Hali hii inachochea taharuki kwa hadhira. Hii ni baada ya Kulia na Kushoto kutazamana uso kwa uso na kukiri kuwa nchi ni tamu kuliko siasa. Haijulikani kama wawili hawa baada ya kubandukana, kujitambua na kutoweka gizani watakubali kuzika tofauti zao ili washirikiane na kujitolea mhanga kwa manufaa ya nchi.

Katika onyesho la pili:

*Giza totoro*! (uk. 26)

(... *Sasa taa zimewaka polepole mpaka anga kali linamiliki jukwaa.* ) (uk. 26)

Giza totoro linaashiria uovu ambao umegubika kasri hili kwani hakuna aliye na uhuru wa kutenda au kusema. Hatimaye anga kali linaiangazia familia ya Mzee Binafsi ikiwa mezani ili iweze kuonekana vyema na hadhira.

**Giza** (uk. 43)

Giza hili linatokea mwisho wa onyesho la pili baada ya mke wa Bw. Binafsi na wanawe kutoka nyumbani kwa kukerwa na udhalimu aliotendewa Mpya. Hali hi inachochea

taharuki kwa hadhira ambayo inabaki ikijiuliza ni yapi yatakayowapata kutokana na hatua hii ya ujasiri.

(*Wanaondoka na kupotea gizani.*) (uk. 55)

**Giza.**

Hali hii inachochea taharuki kwa hadhira. Mwisho wa onyesho la pili, wana wa Bw. Binafsi, wamekubaliana kushirikiana na umma katika kusema ukweli. Wameenda mafichoni kupanga njama.

**Giza** (uk. 70)

Giza hili linaashiria mwisho wa onyesho la tano. Hali hii pia inaashiria fumbo na hali ya kuubeza uongozi wa Bw. Binafsi. Washiriki wake Bw. Naona na Bw. Salimina wanaonekana kushindwa na hata kutambua nguvu za umma. Bw. Naona anaona kundi kubwa la watu kutoka sekta na hadhi mbalimbali na linalojua na kutambua. Ya mno ni kuwa watoto watatu wa nyumba kubwa ndio waasisi, wa fikiria hizi mpya.

Katika onyesho la sita:

**Giza** (uk.75)

Huu ni mwisho wa onyesho la sita. Hali hii inaendelea kubuni taharuki na mabadiliko ya hisia kwa hadhira. Sasa kuna matumaini kwani sauti ya umma imetangaza kutosita mpaka sauti zao zisikike.

**Giza** ( uk. 82)

Mwisho wa onyesho la saba, mambo si shwari tena. Kuna mabadiliko ya hisia kwa Bw. Binafsi. Ana hofu kwani amejipata katika mazaji ya kutamauka baada ya kushauriwa na yoo ajiuzulu.

**Giza** ( uk. 88)

Giza hili linaashiria mwisho wa onyesho la nane. Utawala wa Bw. Binafsi umefika kikomo. Ana hofu na kuona aibu na anatamani ardhi ipasuke yeye na mkewe waingie. Anatamani jumba liporomoke kama utawala wake. Amekataliwa na umma wakiongozwa na wanawe na hajui hatima yake.

Mtunzi Mohamed amekitumia kipengele hiki cha uangazaji kuiwezesha hadhira kuona yale yanayoigizwa kwenye jukwaa. Giza, mwangaza hafifu na hata mwangaza uliong'aa ni mambo ambayo yametumika kuwasilisha ujumbe wa tamthilia kama vile mabadiliko ya hisia, hofu, fumbo, mazaji, kukosa msimamo, uovu, wasiwasi na matumaini ya haki na ukombozi. Giza pia limeonyesha mwisho wa onyesho moja ili kupisha lingine.

### 3.1.5 Sauti

Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele hiki cha sauti katika tamthilia ya K*imya Kimya Kimya.*

Katika kifunguzi:

(*... anaisikia sauti inayotoka kisimani ...* ) (uk. 8)

**Sauti ndani ya kisima:** *Hakuna uhai. Hakuna chakula. Hakuna maji.*
*Hakuna ari ya kusema. Hakuna shime ya kutenda.*
*Hakuna mori wa kukataa. Hakuna ushinde wa*
*kushindana na kuchachamaa ili kujikwamua...*
*Tazama mbele, usitazame nyuma.. Ijali tamu*

*ya nchi yako, usijali tamu ya siasa tupu.*

*Ijali nchi na kuitetea.*(uk.8)

**Sauti ndani**

**ya kisima:** *Ulikopita kote kukavu. Kote kumedamirika. Hakuoti kitu. Hakuzai kitu. Huko nafsi za watu zimefifia ari. Hata ya kusema neno moja la kweli, neno moja la kweli, neno moja la utetezi... Tazama mbele, usitazame nyuma. Ijali tamu ya nchi yako usijali tamu ya siasa.* (uk. 11)

Sauti ya kwanza inamhimiza mhusika Kushoto huku ya pili ikimhimiza mhusika Kulia. Wawili hawa wanahimizwa watupilie mbali tofauti zao za kibinafsi ili washirikiane kuikomboa nchi kutokana na uongozi mbaya ambao ni chanzo cha matatizo ambayo kila mmoja wao ameyashuhudia alikotoka. Wanahimizwa kuitazama hali hii ambayo inaashiriwa na kisima hiki kinachosema na kilichokuwa kikibubujika maji na uhai lakini sasa ni kikavu.

Katika onyesho la kwanza:

**Sauti ndani**

**ya kisima:** *Ishara njema... Ishara njema... Ishara njema... Njema, njema, njema, ishara njema. Tulikutaraji. Sasa wakati umeshafika. Njoo*

*uliyekuwa ukitarajiwa. Njoo uliyengojewa.*

*Njoo kwa uhakika, njoo tukunyweshe maji ya*

*ujasiri. Ingia ndani ya kisima, uogelee na*

*kujisuuza.* (uk. 21)

Sauti hii inamlenga mhusika Mpya msichana mdogo na mwenye ujasiri ambaye tayari amejikomboa kimawazo na kutambua kuwa wakati wa kusema umewadia. Sauti kutoka kisima hiki ambacho ni amali ya jamii inamkaribisha akabidhiwe na miungu nguvu za kuiongoza jamii katika kujikomboa.

(*... Unazuka mkemeo na mkaripio mkali unaojaribu*

*kuamrisha hadhira...*) ( uk.26)

(*... Mkemeo na mkaripio mkali zaidi unaamrisha hadhira*)

(uk. 26)

(*... Ghafla chuma kinaanguka sakafuni pahala fulani kwa*

*mpasuko mkali unaopasua vigoma vya masikio*) (uk. 27)

**Sauti :** Nani huyo?

(*Sauti inakaripia nyuma ya jukwaa.*) ( uk. 27)

**Sauti:** A-a Bi. Mpya, hapa kwenu watu hawasemi waziwazi kwa kelele. Hawaruhusiwi kufanya hivyo (uk. 27)

**Sauti:** Wewe ni nani? (uk. 28)

**Sauti:** Hapana wewe ni raia wa familia hii inayoongoza nchi. Wewe ni mtoto wa Mzee Binafsi, babako na Bi. Shoo mamako. (uk. 28)

**Sauti:** Kikaango tokea lini kikasema? (uk. 28)

**Sauti:** Hatari! Au labda ajali. Shauri upepo umeanza kuvuma. Aaa – labda ajali ...( ... *vitu vingine vinaanguka kwa mshindo mkubwa na kwa sauti kali*?.) (uk .28)

(*Anasikika akifunga dirisha.*) (uk. 29)

Familia ya Bw. Binafsi iko mezani. Sauti ya mkemeo ni mwangwi wa Bw. Binafsi akiwanyamazisha watu wote ndani na nje kudhihirisha jinsi Bw. Binafsi alivyowanyima watu uhuru wa kuongea kwake nyumbani na hata nje. Mkemeo unasikika kabla familia ya Bw. Binafsi kuonekana kwenye jukwaa. Sauti zinazosikika nje ya jukwaa zikijibizana kama vile sauti ya kikaango kuanguka kwa mshindo zinamkejeli Bw. Binafsi. Hana uwezo wa kuviadhibu vyuma au upepo unaovuma na kuviangusha. Mpya anaihakikishia sauti hii kwamba ingawa amezaliwa katika nyumba kubwa, yeye ni mwananchi, mzalendo na mkereketwa. Mpishi anajaribu kuuzuia upepo kwa kulifunga dirisha ili asifutwe kazi. Huyu ni kielelezo cha wanaojali masilahi yao pekee.

(*...Lakini inasikika kutoka nyuma ya jukwaa*) (uk .30)

Mhusika Mpya anatazama hewani na kuirusha sauti yake kuielekeza hadhira kupitia zile nguvu alizopewa na wahenga katika kile kisima cha maji ya ujasiri.

**Sauti ya Mpya :** Huyu ndiye babangu ... (uk. 30)

**Sauti ya**

**Mpya:** ( *Inanatoka nyuma ya jukwaa*) ( uk..32)

Tazama mamangu ameketi katika ukingo wa dunia. Ana hofu za kuanguka na kuangamia … (uk.32)

(*… Sauti yake Mpya inasikika na hadhira lakini yeye haonekani kusema …*) (uk. *32)*

*Hakisikiki kitu ila midundo ya mioyo na mlio wa saa pahala fulani.* (uk.33)

*(Hasemi, lakini sauti yake inatoka nyuma ya jukwaa na anayeisikia ni baba mtu tu.*)

(uk. 39)

(*Kicheko cha Mpya ) Ha,ha, ha,ha…* (uk. 40)

Mwangwi wa sauti ya Mpya inawakashifu wazazi wake ambao wanayajali mahitaji yao tu. Sauti inayotolewa na midundo ya mioyo na mlio wa saa ni dhihirisho kwamba hakuna anayezungumza mahali pale. Kicheko cha kejeli kinatokea nyuma ya jukwaa wakati Bw. Binafsi anajigamba kuwa yeye ndiye kiongozi wa nyumba na nje.

(*Sauti kali za maporomoko ya vitu vingi vya chuma jikoni …*) ( uk.43)

Sauti hii inakashifu maneno ya Bw. Binafsi kuwa familia yake italaaniwa na kukosa radhi zake kwani anayestahili laana ni yeye kwa kuwadhulumu walio chini ya uongozi wake.

Katika onyesho la tatu:

**Sauti ya**

**Mpya :** (*Ghafla sauti ya Mpya inazuka na kuenea chumbani mwa akina Mussa na Zanga.*)

(uk. 49)

**Sauti ya**

**Mpya:** (*Sauti inatokea nyuma ya jukwaa.*) Kila siku vitu huanza kama mchezo. Kama wasemavyo wazee; mwanzo wa ngoma ni lele...) (uk. 51)

**Sauti ya**

**Mpya:** *Kaka Mussa... siku hizi watoto huzaliwa wakiwa watu wazima...*( uk. 51 – 53)

**Sauti ya**

**Mpya:** Ndani na nje ya majumbani mwetu ni sawasawa. Hakuna tafauti. Wanaotawala ndani na nje ni baba zetu. Nje kunakandamizwa kama tunavyokandamizwa ndani...(uk. 53)

Katika onyesho la tatu:

**Sauti ya**

**Mpya:** Kweli kuliko kweli yoyote...( uk. 54)

" Sasa wanaojua ni wengi kuliko wasiojua.(uk.55 )

Katika onyesho la nne:

(*Wanaimba polepole ...)* (uk. 61)

Athari za tambiko alilofanyiwa Mpya zinabainika kwa sababu sauti yake iliyoenea inasikika wazi ikivikashifu vitendo vya babake na hata mamake anayeijali tu ndoa yake. Sauti ya Mpya inamkumbusha Mussa kuwa hata ingawa yeye ana umri mdogo ana uwezo

wa kuona na kuelewa majanga yanayowaelemea. Mengi ya majanga haya yanaendelezwa na wazazi wao. Anasema kuwa katika maisha yake yote amekoseshwa haki ya kusema mpaka pale alipoambukizwa uchawi wa wazuka katika yale maji ya kisima cha ujasiri. Mpya na Zanga wamefaulu katika kumzindua kaka yao Mussa. Kuna matumaini kwa sababu idadi ya waliozinduka inaendelea kuongezeka. Wimbo wanaoimba wananchi katika uwanja wa Bustani wakiongozwa na Mpya na kaka zake ni mwito unaowaongoza na kuwaunganisha.

Katika onyesho la sita:

**Sauti ya Mpya:** *Sisi wananchi tumeamua kwamba kesho tukutanike tena kulalamika na kutetea haki zetu....*(uk. 72-73)

**Sauti ya umma:** Tumekubali. Tumekubali yote. Tuko pamoja na wewe... (uk. 73)

**Sauti ya Mpya:** Muhimu kabisa katika yote, kwanza ni kupitia katiba yetu... (uk. 73)

Sauti hizi zimekubaliana kuendelea kupigania haki kwa imani bila kutamauka.

**Sauti ya umma:** Sauti yako inatueleza tunayoyajua sauti

yako ni sauti yetu… (uk. 75)

**Wimbo:** Haki ni kama upanga…Usipoitekeleza utajutia… (uk. 77)

(… *Kicheko kisichojulikana wapi kinatoka kinaenea katika mazingira ya hapo)* (uk. 78)

Katika (uk. 80)

**Sauti ya Mpya:** Taifa lazima likogeshwe.

**Sauti ya wananchi:** Taifa lazima lisuguliwe.

**Sauti ya Mpya :** Taifa lazima litakaswe.

**Sauti ya wananchi:** Taifa lazima lisafishwe.

**Sauti ya Mpya:** Polepole wananchi, bila zogo.

**Sauti ya wananchi:** Taratibu wananchi, taratibu.

**Sauti ya Mpya:** Mko sawa wananchi mko sawa?

**Sauti ya wananchi:** Tuko sawa, tuko sawa kabisa… (uk. 80)

Sauti ya Mpya inajibizana na sauti ya umma ambayo imemuunga mkono katika utekelezaji wa jukumu la kubadili mambo na kubuni sera za kuleta mabadiliko katika nchi yao. Wanatarajia kutimiza haya kwa kuipitia katiba kwa mujibu wa mahitaji ya kisasa, kugeuza mwenendo wa kutojali masilahi ya kitaifa, kuhakikisha wananchi wanahudumiwa, kuondoa ufisadi na kuzilinda rasilmali za nchi. Sauti hizi zinajibizana baada ya Bw. Binafsi kuwafukuza washiriki wake Bw. Naona na Bw. Salimina kutoka ofisi yake. Kicheko kinasikika kikimkejeli Bw. Binafsi anayejaribu kuinyamazisha hadhira.

| | |
|---|---|
| **Sauti ya Yoo:** | Nilikwambia zamani mwenendo wako ukanidharau… (uk. 82) |
| " | Sasa? Sasa hapana cha sasa, hapana ila uji… (uk.82) |
| " | Ikiwa ni hivyo, basi mimi sitasema tena. (uk. 82) |

Sauti ya Yoo inamshauri ajiuzulu ilhali yeye anashindwa vipi na utawala ni wake pekee. Huu ni mvutano wa hisia. Bw. Binafsi hana budi kujitazama kwenye kioo kikubwa kinachoakisi matendo yake kama kiongozi. Anazungumza na nafsi yake kupitia sauti ya yoo. Dhamiri yake inamkumbusha kuwa alistahili kutawala kwa wema lakini akapuuza. Sasa miungu wametoa hukumu na watoto wake wameongoza harakati za kumng'oa mamlakani. Nafsi moja inamshauri ajiuzulu huku nyingine ikishikilia kuwa utawala huo ni wake pekee.

Katika onyesho la nane:

| | |
|---|---|
| **Sauti za wananchi:** | Tunadai haki zetu. Tumesubiri, tumesubiri zaidi ya miaka hamsini hakuna la maana... (uk. 84) |
| " | Mchezo umekwisha. Umefika mwisho. (uk. 87) |

Hizi ni sauti za wananchi ambao tayari wamelizunguka kasri la Bw. Binafsi kumtoa mamlakani. Mchezo wake wa kuwanyamazisha watu na kujiwekea ulinzi mkali ili kuhifadhi cheo umekoma. Kipengele hiki ambacho hakionekani pia kimetumiwa na mtunzi kwa upana na ubunifu mkubwa. Kuna sauti za wahusika zinazosikika bila wao kuonekana wakizungumza kama vile sauti ya mhusika Mpya na sauti za watu ambazo zinasikika nje ya jukwaa. Kuna sauti ambazo zinadaiwa na matini kama vile sauti ndani ya kisima, sauti ya Yoo na sauti inayosikika mpishi anapofunga dirisha jikoni baada ya sauti ya vyuma vinavyoanguka kusikika. Sauti hizi ni za kufanikisha uigizaji kwenye jukwaa.

### 3.1.6 Kimya

Kipengele hiki kimekaririwa mara tatu ili kuipa tamthilia anwani, K*imya Kimya Kimya.* Sehemu hii inachunguza matumizi ya kipengele hiki katika kazi hii ya sanaa.

(*Kimya. Halafu...*) (uk. 14)

(…*Kimya, kisha.*) (uk. 15)

Kimya hiki katika kifunguzi ni baada ya mhusika Kushoto kumwambia mhusika Kulia kuwa pale kisimani hakupata maji bali amepata kujiona nafsi yake ambayo ni mbaya na lazima aisafishe. Wahusika hawa wanakaribiana nyuso katika juhudi za kufahamiana kwa kuchunguzana kwa makini.

Katika onyesho la kwanza:

(…, *Kimya kimya* ….) ( uk. 22)

Mhusika Mpya anaelekea kisimani polepole baada ya kusikia sauti kutoka ndani ya kisima ikimkaribisha anyweshwe maji ya ujasiri. Kimya hiki kinachimuza umuhimu wa kisima hiki. Hii ni amali ya jamii ambapo wahenga wanazungumza na jamii kupitia kisima hiki ambacho pia ni kielelezo cha nchi.

Katika onyesho la pili:

(… *Kimya* …. ) (uk. 26)

(…*Halafu Kimya*) (uk. 27)

Kimya hiki kinatokea mara tu sauti inapokaripia nyuma ya jukwa baada ya chuma kuanguka sakafuni pahala fulani kwa mpasuko mkali. Kimya hiki kinasisitiza kuwa hakuna anayethubutu kutoa sauti katika nchi hii.

(*Kimya! Baadaye upepo…*) (uk. 28)

(… *Kimya…*) (uk. 29)

(… *Kimya!* … *Kimya, Kimya Kimya* ….) (uk. 33)

(... *wote wanakaa Kimya kwa muda...*) ( uk. 34)

(*Kimya......*) (uk.35)

(*Kimya. Halafu....*) (uk. 37)

(*Kimya halafu...*) (uk. 38)

Kimya katika sehemu hii kinabainisha hali ilivyo kwa Bw. Binafsi wakati familia yake iko mezani wakisubiri baba mtu. Yeye ni kikwazo kwa yeyote aliye chini ya himaya yake. Kimya kinatokea na baadaye upepo unavuma kuonyesha kuwa kuna nguvu ambazo Bw. Binafsi hawezi kuzidhibiti wala kuzipinga kwa kutumia askari wake na virungu vyao. Kimya kinaipa hadhira nafasi ya kusikia sauti nje ya jukwaa zinazosababishwa na kuanguka vyuma na kuona athari ya sauti hizi kwa jamii hii. Kimya pia kinatokea baada ya kila mwanafamilia kuungama utiifu wake kama ilivyo desturi. Hapa hadhira inapewa nafasi ya kutathmini utiifu huu. Mpya anajipata mashakani kwa kulalamika badala ya kutii.

(*Kimya, halafu...*) (uk. 52)

Huu ni wakati sauti ya Mpya inaposema na Mussa na kumhakikishia kuwa umri wake mdogo haumzuii kujua tofauti kati ya uongozi mbaya na mzuri na hata kuzijua haki zake. Katika onyesho la tano:

(*Kimya..* ) (uk. 65)

(... *Kimya .. wanaonekana wanatafuta jibu mwafaka kimyakimya...* ) (uk. 67)

(*Kimya...* ) (uk. 69)

Kimya kinachotokea katika onyesho hili kinaipa hadhira nafasi ya kuwaza. Bw. Naona

waziri wa nchi na Bw. Salimina ofisa wa usalama wanashindwa jinsi watakavyomwambia Bw. Binafsi habari za kuatua moyo kwamba wanawe ndio wasisi wa fikra mpya. Bw. Salimina, afisa wa usalama anakubaliana na Bw. Binafsi kwa kinaya kuwa hakuna taifa jingine duniani ambalo linajulikana kwa huduma bora na ambalo watu wake hawasemi ovyo. Bw. Binafsi hakubaliani na washirika wake hao wawili kuwa kuna kikundi cha maana kisicho na uongozi kinachoweza kukusanyika na kuandamana. Mkusanyiko huu kama anavyodai Bw. Salimina unajiongoza kwa mawimbi na mishikamano ya pamoja yenye mvuto kama sumaku. Hii ni taswira ya kizazi kipya kinachotumia teknolojia ya kisasa kuwasiliana.

Katika onyesho la tano:

(*Kimya kinadhihiri*) (uk. 78)

Katika onyesho la nane:

(*Kimya tena…*) ( uk. 81)

Kimya hiki kinatokea wakati Bw. Binafsi anaomboleza na kusema na Yoo baada ya kushindwa kuinyamazisha hadhira na kutambua kwamba hana budi kuwapa walio wengi.

(*Kimya. Kimya kirefu kidogo …* ) ( uk. 82)

Kimya hiki ni kabla ya sauti ya Yoo kumjibu Bw. Binafsi ili kuchimuza yatakayotokea baadaye kuweza kuwaziwa kwa makini.

(Kimya, halafu.. ) (uk. 87)

Kimya kinatokea baada ya Bw. Binafsi kuliendea yoo kwa huzuni. Kupitia hili yoo anataka nafsi yake imhakiki, imkejeli imtusi, imshambulie na hata kumlaumu. Anatafuta suluhuhisho wakati maji tayari yamemwagika.

Kimya kimetumika katika tamthilia kusisitiza ujumbe wa tamthilia. Kipengele hiki kimetumiwa na mwandishi ili kuwawezesha waigizaji kuweza kuwasilisha ujumbe kwenye jukwaa kupitia uigizaji.

### 3.1.7 Mihimili

Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele cha mhimili katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya.*

Katika kifunguzi:

> (...*wanakutana kwenye kisima kikavu cha maji*
>
> *yasiyotekeka.*) (uk.8)

Kisima hiki ni nguzo muhimu katika tamthilia hii na ingawa ni ishara ya uhai, ni kitupu. Kisima hiki ni amali ya jamii ambapo suluhisho la matatizo yanayoikumba jamii yatapatikana. Vile vile kisima hiki ni kielelezo cha nchi ambayo wananchi wake wamepoteza matumaini ya kuishi kutokana na uongozi mbaya.

Katika onyesho la kwanza:

> (...*Taratibu anaibuka huku kanyanyua mikono*
>
> *inayonyanyua bakuli la maji.*) (uk. 23)

Bakuli hili la maji linaashiria kiamo cha kuteka maji ya ujasiri. Hili ni tambiko la uhai wa nchi kwani litamwezesha mhusika Mpya kusema kwa niaba ya jamii bila hofu. Ukombozi hauna budi kuhusishwa na mbinu ambazo mababu zetu walitumia kukabiliana na maovu.

Katika onyesho la pili:

*( … Familia ya Mzee Binafsi iko mezani… meza iliyojaa vyakula vya kila aina… ghafla chuma kinaanguka sakafuni…)* (uk. 27)

Meza na viti vilivyokaliwa na familia hii vinadokeza ukosefu wa uhuru na utangamano unao hitajika katika jamii. Mpya anaonekana ametengwa huku Bw. Binafsi akitengewa kiti maalum. Meza iliyojaa vyakula vya kila aina ni ishara ya utajiri lakini badala ya furaha kuna hofu. Kikaango cha chuma kinachoanguka sakafuni huko jikoni kwa mpasuko kinaashiria maasi na kuporomoka kwa utawala wa Bw. Binafsi. Hakuna mtu au kitu kinachoruhusiwa kusema. Sio watu tu ambao wana kiu ya kusema hata vifaa vingine. Sauti hizi zinamkera Bw. binafsi kwa kumkejeli.

*(…ila midundo ya mioyo na mlio wa saa…)* (uk.33)

Saa imetumika ili kudhihirisha kimya ambacho kimekithiri na pia kumkejeli Bw. Binafsi kwani katika nyumba hii kuna vitu visivyotii amri yake. Midundo ya mioyo inaweza tu kusikika palipo na kimya cha kupindukia na haiwezi kuzuilika.

Katika onyesho la tatu :

*(...Chumba chenye vitanda vya kisasa…samani na mapambo …)* (uk.45)

Vitanda vya kisasa, samani na mapambo ni mihimili ya kudhihirisha utajiri.

*(…Sasa amechukua mto …)* (uk.46)

Mto huu unatumiwa na Mussa kuzuia sauti ili kubainisha ukosefu wa uhuru wa kusema.

*(Anainuka pale penye kiburunji…)* (uk.57)

Mhusika Bw. Sikilivu na wenzake wanajaribu kupitisha wakati wa kucheza mchezo wa mawe wakisubiri mkutano wa dharura katika bustani ya taifa kijijini. Hii ndiyo njia ya pekee ya kujistarehesha kwa mwananchi wa kawaida.

Katika onyesho la nne:

(...*Na kuingia na virungu vyao*...) (uk.61)

Virungu hivi vya askari vinadhihirisha dhuluma kutoka kwa kiongozi duni asiye na kipawa cha kuongoza katika harakati za kuhifadhi cheo.

Katika onyesho la saba:

(...*Anaanza kuomboleza na kuliambia yoo*...) (uk.81)

Yoo ni kioo kikubwa ambacho Bw. Binafsi anatumia kujitazama nafsi yake liyokengeuka na kutumia muda mwingi kujihalalishia na kudumisha uongozi. Kioo hiki kinaakisi matendo yake yote kama kiongozi.

Katika onyesho la nane:

(*Bw. Binafsi na Bi. Shoo wamebwatika juu ya sofa*...) (uk.84)

Sofa ni ishara ya starehe ilhali nyuso za wawili hawa zimesawijika kwa hofu.

(*Kundi la watu wanaobeba mabango*...) (uk.84)

Mabango haya ndio yanayosema mahitaji ya wananchi. Bw. Binafsi na washirika wake wayasome kimya kimya kwani hawataki kusikia watu wakisema kwa sauti. Kimya kinasema kimya kimya kwa sauti kubwa kama ya Yoo. Hii ndiyo mbinu mwafaka sasa.

Mtunzi wa tamthilia hii ametumia mihimili au viambata jukwaa katika kazi yake ili kufaulisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa.

## 3.2 Hitimisho

Katika sura hii tumevitathmini vipengele vya utendaji katika tamthilia ya K*imya Kimya Kimya* ambavyo ni mandhari,maleba, miondoko, uangazaj, kimya, sauti na mihimili. Tathmini yetu imeibainisha kwamba mtunzi wa tamthilia hii ya *Kimya Kimya Kimya* amevihusisha vipengele vya utendaji katika kazi yake

# SURA YA NNE

## 4.0. Vipengele vya Utendaji katika Tamthilia ya *Sudana.*

Katika sura hii tumevitathmini vipengele vinavyofanikisha utendaji katika tamthilia ya *Sudana.* Tamthilia ya *Sudana* inahusu matatizo ya chombo baharini yanayopelekea wahusika Sudana, Shume, Sizwe, Sudzungu na Mabaharia Wazanji kujikuta mikononi mwa mabaharia Wamerope, Amerigo na Muzungu. Hawa washirika wawili ni watu ambao matendo, tabia na hatua zao zinatawaliwa na imani, mielekeo na taasubi kali. Sudana anatatizika baina ya kuilinda hadhi yake kwa upande mmoja na kuiuza hadhi hiyo kwa upande mwingine ili kuwanusuru wanawe wasiangamizwe katika madhila na mzigo wanaotwikwa na Amerigo na Muzungu. Kuna maingiliano changamano kati ya pande hizi mbili. Tumevichunguza vipengele vinavyofanikisha utendaji navyo ni: mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili.

### 4.1. Maelekezo ya Jukwaa

Kipengele hiki muhimu cha utendaji kimeshughulikia mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili. Hii ni kwa sababu tamthilia ya *Sudana* kama tamthilia zingine haina maelezo na simulizi zinazopatikana katika riwaya au hadithi fupi bali kuna utendaji unaosimamia maelezo na simulizi.

#### 4.1.1. Mandhari.

Ni muhimu kuzingatia kipengele hiki cha uigizaji ili kupata taswira ya mchezo kama wanavyoeleza Griffiths na Hemming (1984). Sehemu hii inatathmini kipengele hiki katika tamthilia ya *Sudana.*

Katika utangulizi:

(... *Wamekaa kwenye deki ya Amerope... Nyavu, makasia, nanga na ala nyingine za kibaharia zaonekana dekini.*) (uk. 7)

(... *Wanaonekana dekini...*) (uk. 16)

Maelekezo haya katika utangulizi yanaonyesha mandhari waliomo mabaharia Wazanji wakizungumza kuhusu matatizo wanayopitia mikononi mwa mabaharia Wamerope. Kulingana na wimbo wao, walijipata katika hali hii ya utumwa baada ya kuibwa zamani na maharamia kisha kuuzwa humo melini mwa bepari uzunguni. Hii ni taswira ya jinsi nchi nyingi katika bara la Afrika zilivyonaswa kwenye mtego na kufanywa watumwa.

Katika tendo la pili, onyesho la 2:

(*Katika chumba cha Amerigo Sudana amekaa kitandani na Sudzungu amekaa kitini akimkabili Sudana.*) (uk. 22)

(*Katika chumba cha Amerigo, Sudana bado yupo kitandani amefungwa silisili. Amerigo ameketi kitini na Muzungu na Sudzungu wamesimama ubavuni mwake. Mbele yao wamesimama Wazanji watatu mmoja akiwa Sizwe, pingu mikononi, wakilindwa na Wamerope waliokamata bunduki.*) (uk. 32)

Mandhari yanabadilika na kuwa katika chumba cha Amerigo. Sudzungu yuko hapa kumsaliti ndugu yake Sizwe kwa kuwasilisha mashtaka ya kuwa na kiburi cha kukataa kuivunja mashua ya Wazanji ili kupata vifaa vya kuikarabati mashua ya Wamerope. Yeye ni kielelezo cha mwananchi mwenye ubinafsi na ambaye amekosa maadili kiasi

cha kuuza utu na nchi. Sudana amefungwa silisili kuonyesha kuwa Amerigo ameamua kutumia nguvu na vitisho kumshawishi Sudana baada ya ushawishi wa Sudzungu kukosa kufaulu. Sizwe ambaye ameonyesha dalili za kuwa tisho kwa kuzinduka amedhibitiwa kwa kufungwa pingu.

Katika tendo la tatu, onyesho la 1:

> (*Shume amekaa kitandani… mbele yake wamesimama wenzake Wazanji wakimtazama.*) (uk. 45)

Mandhari haya ni katika chumba kimoja katika mashua na yanambainisha mhusika Shume baada ya kujeruhiwa bega kwa risasi aliyofyatuliwa na Amerigo baada ya kumfumania akijaribu kumnajisi mamake. Shume ni kielelezo cha mtu ambaye yuko tayari kujitolea mhanga ili kuilinda nchi yake dhidi ya najisi.

Katika tendo la tatu, onyesho la 2:

> *(Amerigo na Muzungu wameketi vitini, na mabaharia wengine Wamerope wamesimama nyuma yao. Upande mwingine wa Jukwaa wamesimama Shume, Sudana na Wazanji wengine pamoja na ngoma na marimba yao. Shume ameshika upanga mkononi.*) (uk. 51)

Haya ni mandhari yanayoonyesha Wazanji wakiwa tayari kucheza ngoma ya toba ili kumwezesha Shume amuombe Amerigo msamaha. Kinaya ni kwamba Shume ndiye amekosewa. Milio na mapigo ya ngoma miongoni mwa Waafrika yaliwasilisha ujumbe uliofahamika na jamii husika hivyo basi bila shaka ngoma hii ya Wazanji ilikuwa na ujumbe muhimu.

Mandhari katika tamthilia ya *Sudana* yamesalia kuwa katika mashua na vyumba katika mashua. Hii ni kwa sababu matukio yote yametendeka katika chombo baharini. Hivyo basi waigizaji hawana budi kujibana katika mazingira haya katika kuwasilisha ujumbe jukwaani.

### 4.1.2 Maleba

Mavazi haya yanayovaliwa na waigizaji hufanikisha uigizaji katika jukwaa hivyo basi sehemu hii inatathimini matumizi ya kipengele hiki katika tamthilia ya *Sudana.*

Katika utangulizi:

> (*...amevaa kanzu ndefu nyeupe iliyozungukwa na mchoro wa ramani ya Afrika. Mipaka ya nje ya ramani hiyo ni myeusi na mipaka ya nchi mbalimbali ni matone na michuruziko myekundu.*) (uk. 1)

Hivi ndivyo mhusika Sudana alivyovalia. Yeye ni kielelezo cha bara la Afrika. Vazi hili linaakisi ujumbe wa tamthilia. Mipaka myeusi ni kielelezo cha Mwafrika huku michirizo myekundu ikiashiria mshikamano wa Waafrika na damu iliyomwagika katika harakati za kupigania uhuru.

> (*... Amerigo amevalia kama haramia wa baharini na Muzungu amevalia kinevi. Kichwani, Amerigo amejifunga kitambaa chekundu. Wote wawili wamejifunga upanga na bastola kiunoni. Darubini inaning'inia shingoni mwa Muzungu...*) (uk. 9)

Amerigo ndiye nahodha wa mashua ya Amerope na Muzungu ni naibu wake. Mavazi ya kiharamia na ya kinevi, kitambaa chekundu, upanga na bastola kiunoni pamoja na darubini ni maleba pamoja na vifuasi na yanatoa picha halisi ya wahusika hawa na kufanikisha uigaji wao kwenye jukwaa. Mabaharia hawa makaburu ambao wanatumia hila na hata nguvu kuwateka Waafrika wamejihami kwa silaha hatari ili kujilinda dhidi ya pingamizi. Mavazi ya Amerigo ambaye amevalia kama haramia yanadhihirisha uharamia na kutoaminika huku kitambaa chekundu kikiashiria hatari na maovu ambayo yametawala mawazo yake. Mavazi ya Muzungu aliyevalia kama mwanamaji yanaonyesha ya kwamba yeye ana ujuzi katika safari za baharini. Darubini inawawezesha kuona mawindo na adui kwa mbali.

(… *Nguo zao zaonekana zimerowa maji na kila anayeingia anapewa nguo za kujifunika.*) ( uk. 12)

Hawa ni abiria wa mashua ya Zinji iliyookolewa na mashua ya Amerigo na Muzungu. Ishara hii ya ukarimu inatumika kama unafiki wa kuwafumba macho Wazanji.

(… *Nywele matimutimu na nguo zimechanika…*) (uk. 47)

Hii ndiyo hali ya Sudana baada ya kunajisiwa na Amerigo. Nywele na nguo zake zinaashiria upweke na utupu baada ya kupokonywa utu. Hii ndiyo taswira ya nchi za kiafrika na raia wake baada ya kuondolewa kwenye amali zao na kukengeushwa na mila za kigeni.

Watunzi wa tamthilia hii wamekitumia kipengele hiki kuchimuza ujumbe na pia kuonyesha tofauti kati ya Wamerope na Wazanji ili ujumbe uigizike kwenye jukwaa.

### 4.1.3. Miondoko

Sehemu hii inatathmini miondoko katika tamthilia ya *Sudana.*

Katika utangulizi:

> (*Sudana anaingia … anasogea mbele ya jukwaa na kuwakabili watazamaji… watu watatu wanaingia na kuanza kucheza na kuigiza, kwa vitendo…*) (uk. 1)
>
> *(Akiwanyoshea mikono watazamaji.)* (uk. 1)
>
> *(Sudana anawanyoshea tena watazamaji mikono kama anayetaka kuwakumbatia, halafu anarudi kinyumenyume mpaka anatoka. Wachezaji watatu nao wanatoka huku wakicheza…)* (uk. 6)

Hii ni sehemu ya utangulizi Sudana, kielelezo cha bara la Afrika anatoa masimulizi kuhusu wanawe ulimwenguni. Anawakumbusha kuhusu matatizo yao kutokana na kutawanywa na kukengeushwa. Anawakumbusha asili yao na pia mshikamano wao utakaowakomboa. Watu watatu wanaocheza na kuigiza wanawakilisha pembe tatu za ramani ya bara la Afrika. Kutaka kuwakumbatia watazamaji ni ishara ya mapenzi kwa wanawe, waafrika.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 1:

> (*… wakitia tanga viraka…*) (uk. 7)
>
> *(Amerigo na Muzungu wanaingia….Wakiongeza bidii katika kazi yao… Amerigo na Muzungu wanatazamana na Wazanji kwa muda.)* (uk. 9)

(*Kwa hasira kidogo.*) (uk. 10)

(*Anamgeukia Muzungu.*) (uk. 10)

(*Wanasogea mbele kidogo wakielekea mlango wa pili wa jukwaa. Amerigo anasimama, na anamsimamisha Muzungu kwa kumkamata bega. Amerigo anaonekana anatazama mbali. Anatoa kijaluba cha tumbaku mfukoni; anakifungua, anatoa tumbaku kidogo na kuitia mdomoni, halafu anakirudisha kijaluba mfukoni. Wazanji wanaendelea kutia viraka*) (uk. 10).

*(Akinyosha kidole.*) (uk. 10)

*(Anaangaza macho.*) uk. 10)

Wazanji wako katika harakati za kuwatumikia Wamerope kwa kuikarabati mashua. Amerigo anawashuku Wazanji kwa sababu ya kuimba kwao. Amerigo ambaye ni mraibu wa tumbaku anaiona taswira ya umbo la mwanamke kwenye kisiwa naye Muzungu anaiona mashua nyingine iliyovunjikavunjika huku abiria wake wakipunga mikono kama ishara ya kuomba msaada. Wasifu wa mabaharia hawa wawili unadhihirika hapa. Amerigo ametawaliwa na fikira za starehe huku Muzungu akiwa makini katika shughuli zake za kuwinda watumwa.

*(Akinyosha kidole.)* (uk. 11)

(*Wazanji wanaacha kushona, wanasimama nyuma ya Amerigo na Muzungu huku wakinyosha na kuangaza macho anakoashiria Muzungu.*) (uk. 11)

(*Anamrudishia Muzungu darubini, na anaanza kutoa amri.*)

(uk. 11)

*(Wamerope na Wazanji wengine wanatokea, na Wanaendeshana mbio huku na huku wakitekeleza amri za Amerigo. Baada ya muda mfupi wote wanakuja na wanasimama nyuma ya Amerigo na Wazanji nyuma.*) (uk. 11)

(*Akipiga saluti.*) (uk. 12)

*(Mabaharia wachache wanasogea mbele na kurusha kamba kupitia mlango mmoja wa jukwaa…*) (*Mabaharia wengine wanatoka haraka haraka.*) (uk. 12)

*(Mmoja, mmoja wanavutwa kwenye jukwaa kwa kamba. Kwanza anaingia Sudzungu, halafu Shume, Sizwe mabaharia Wazanji wengine na mwisho Sudana ambaye anatazamwa kwa matamanio makubwa na Amerigo.*) (uk. 12)

(*… Sudzungu nahodha wa mashua ya Zinji anawapigia Amerigo na Muzungu saluti. Muzungu anawatazama Sudana na Sudzungu kama anayewakumbuka kwa mbali.*)

(uk. 12)

(*Akijibu saluti*) (uk. 12)

Amerigo kwa kutumia darubini pia aliweza kuiona mashua ndogo iliyovunjikavunjika huku abiria wake wakipunga mikono kama ishara ya kuomba msaada. Harakati za kulipokea windo hili jipya zinaonekana katika mashua ya Wamerope. Kamba iliyotumika kuwaokoa ni ishara ya kifungo chao. Nahodha wa wazanji anapiga saluti kuonyesha

heshima na shukrani kwa niaba ya wenzake, naye Amerigo kwa kuwafumba macho anaijibu saluti na kuikaribisha mashua ya Zinji katika mashua ya Amerope. Anawaeleza kwa kinaya kuwa hii sio mara ya kwanza kutenda kitendo cha ukarimu kama hiki na hivyo basi jambo hili sio geni kwake.

> (*Akimtazama Sudana)*... (*Sudana anatazama chini.*) (uk. 14)
>
> (*Amerigo anaendelea kumtazama Sudana kwa jicho la matamanio, na Sudana naye anaendelea kutazama chini.*) (uk. 14)
>
> (*Anawageukia Wazanji wa Amerope.* ) (uk.14)
>
> (*Wote wanaondoka... Amerigo anatazama Sudana anavyokwenda mpaka anatoka.*) (uk. 14)

Amerigo anamtazama Sudana kwa tamaa naye Sudana anaona haya. Sudana amejipata mwathiriwa mara dufu. Kama mwafrika na kama mwanamke, kiumbe dhaifu cha kumstarehesha mwanamume. Amerigo anamrejelea kama chombo. Anamwambia Muzungu kwamba Sudana ni mashua inayohitaji nahodha kama yeye.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 2 :

> *Wengine wanasafisha deki., wengine wanatengeneza nyavu n.k. ... Amerigo na Muzungu wanaingia.)* (uk. 16)
>
> (*Muzungu anatazama nyuma, Kidole cha shahada mdomoni na macho ameyakodoa akijaribu kuwanyamazisha Wazanji...*) (uk. 18).
>
> (*Wazanji wanarudia kazi yao... Amerigo na Muzungu wanatazamana...*) (uk. 18)

*(Mzanji 4 anaingia mbio huku anahema nyuma yake amefuatwa na Sudzungu).... Muzungu na Amerigo wanageuka kuwatazama. Mzanji 4 anapiga magoti mbele ya Amerigo na Muzungu. Sudzungu anasimama kando yake. Wazanji wengine wanasimamisha kazi na kusogea pale alipo mwenzao)...(anashika kichwa...)* (uk. 19)

(... *Mzanji 4 anatetemeka.*) (uk. 20)

...*(anaanza kuondoka.)* (uk. 20)

*Shume anasogea mbele haraka haraka.*) (uk. 20)

(...*Wanaondoka... Shume na Sizwe wanasimama, wanageuka, wanatazama... halafu wanatoka...* ) (uk. 21)

Wazanji wanaimba huku wakiwatumikia wamerope kwa kufanya kazi. Kazi ya sulubu wanayoifanya ni ya kushurutishwa na haina manufaa yoyote kwao. Wimbo wanaoimba ni mwito unaowaunganisha na kuwaongoza katika kutafuta suluhisho. Muzungu anajaribu kuwanyamazisha kwa ishara ya kidole mdomoni huku akiwaangalia kwa macho makali. Amerigo anamweleza Muzungu anayekerwa na sauti za wimbo kuwa huwezi kuwatenganisha Wazanji na ngoma kwani huo ndio urithi wa pekee waliopata kutoka kwa Mungu. Mzanji 4 anaonyesha hofu ya kuangamia kwani mbao zimeoza huko chini na maji kuanza kuingia. Shume anachukua hatua ya ujasiri ya kumzuia Amerigo kutumia vifaa vya mashua ya ZINJI kutengenezea mashua ya AMEROPE huku vifaa vilivyosalia viwekwe akiba. Makubaliano yalikuwa wasaidiwe kuikarabati mashua yao ili waende zao.

Tendo la pili, onyesho la 1:

…(*Akionyesha matiti yake.*) (uk. 23)

(… *Sudzungu anasimama haraka haraka na kumpigia saluti. Amerigo anavua upanga wake na kuuweka pembeni. Anasogea alipo Sudzungu.*) (uk. 23)

(*Akitabasamu.*) (uk. 23)

(*Anapiga saluti na kutoka. Amerigo anasogea kitandani alipo Sudana na kukaa ukingoni. Anajaribu kumgusa Sudana lakini Sudana anasonga kando.*) (uk. 23)

(*Anamnasihi.)* (uk. 24)

(*Baharia mmoja Mwamerope anaingia ghafla.*) (uk. 23)

(*Kwa hasira zaidi.*) (uk. 23)

(*Akisimama.* ) (uk. 23)

(*Anatoka. Amerigo anashusha pumzi za hasira na kurudi tena kukaa*

*kitandani.*)

( uk. 24)

(*Anajaribu kumgusa Sudana lakini Sudana anamkwepa)*

(uk. 24)

(*Anamkamata mkono Sudana kwa ghafla. Anamshika na kujaribu kumkumbatia. Sudana anajaribu kujitatua. Mwishowe anampiga meno shingoni Amerigo. Amerigo anapiga siyahi na kumwacha Sudana. Sudana anajivuta kando huku Amerigo akitoa kitambaa na kujikanda pale alipoumwa…*) (uk. 25)

*Sudana anaondoka kitandani na kuanza kuzunguka chumbani huku Amerigo akimfuata kwa macho yake.*) (uk. 26)

*(Amerigo anasimama na kuanza kumfuata Sudana. Sudana anarudi kinyumenyume.*) (uk. 27)

Sudana anaonyesha matiti yake kama ishara ya kumlaani mwanawe Sudzungu kwa sababu amekubali kutumiwa na Amerigo kumshawishi na hivyo basi kuwa gawadi wa mamake. Yeye ni kielelezo cha mtu aliyetawaliwa na ubinafsi na tamaa. Sudzungu ana mheshimu Amerigo kwa kumpigia saluti huku akimkosea mamake mzazi heshima. Amerigo anafikiria kuwa Sudana ameshawishika na ndipo anaonyesha furaha na kuridhika anapouweka upanga ukingoni huku akitabasamu. Amerigo anakasirika juhudi zake za kukidhi tamaa yake zinapositishwa na Mwamerope anayeingia ghafla. Amerigo bado anaamini kuwa Sudzungu amefaulu kumshawishi mamake ndipo anaendelea kung'ang'ana. Ukweli huu unamjia mwanamke huyu anapojiitetea kwa meno, silaha ya pekee aliyonayo.

(*Amerigo anamrukia Sudana. Anajaribu kumtumilia nguvu. Wanaanguka huku wakiendelea kumenyana. Sudana amuuma Amerigo sikioni, halafu anampiga teke la tumbo na kumsukuma kando. Sudana anasimama haraka na kukimbilia upanga wa Amerigo ulioko pembeni. Amerigo anasimama na kuanza kurudi kinyumenyume. Wote wawili wanatweta.*) (uk. 27)

(*Kwa hofu*) (uk. 27)

*(Anarudi kinyumenyume kuelekea mlango) …. (Amerigo anatoka mbio … Sudana polepole anarudisha upanga pale alipouchukua.)* (uk. 27)

*(Akiteremsha pumzi.)* ( uk. 27)

*(… Anageuka kwa ghafla. Amerigo anaingi… Wanamrukia Sudana. Sudana anapigana nao mpaka wanamshinda nguvu na hatimaye wanamfunga mikono yake kitandani kwa silisili)* (uk. 28)

(*Mabaharia wanatoka)… (Anampiga Sudana kofi)…(Anaingia Shume. Anamtazama Sudana, halafu anageuza uso na kumtazama Amerigo.*) (uk. 28)

Amerigo anaondoka chumbani kwenda kutafuta msaada baada ya kung'amua ujasiri wa mwanamke huyu ambaye yuko tayari kuhifadhi hadhi yake kwa lolote. Amerigo yuko tayari kutumia mbinu yoyote kukidhi mahitaji yake. Sudana anafungwa silisili ili kudhibitiwa. Ari na ujasiri ni mambo ambayo yanamwezesha kupambana na mabaharia Wamerope wawili.

(*Kwa ukali.*) (uk. 28)

(*Amerigo anatoka kwa hasira. Shume na Sudana wanatazama kidogo. Halafu Shume anachukua viatu anatoa kitambaa kikubwa kutoka kabatini, halafu anakaa kando na kuanza kupangusa viatu vya Amerigo*) (uk. 29)

*(Anaendelea kupangusa viatu.)* (uk. 29)

(*Amerigo anaingia ghafla … Amerigo anapita mbele ya*

*Shume kwa vishindo akimtazama Shume anavyopangusa viatu. Lakini akisha pita tu anasimama ghafla. Anageuka polepole. Anasogea kidogo na kusimama mbele ya Shume.*) (uk. 30)

(*Shume anainua macho kumtazama Amerigo, kisha yeye na Sudana wanatazamana, Wamerope watatu wanaingia, Mmoja amebeba kamba na kiboko.*) (uk. 30)

*(Shume anaweka viatu chini na kusimama.*) (uk. 30)

(*Shume anainama, anakiokota kitambaa na kumpa Amerigo. Amerigo anakipokea kitambaa kwa mkono wa kushoto, na ghafla anampiga kofi Shume kwa mkono wa kulia, Shume anajikutua kama ambaye yuko tayari kupigana, lakini anajizuia. Mabaharia wanasogea haraka haraka karibu na Amerigo, tayari kumlinda. Polepole Amerigo anakikunjua kile kitambaa halafu anakiinua kumwonyesha Shume…*) (uk. 30)

Katika tendo la pili, onyesho la 2:

*Baharia anampa Amerigo kiboko, halafu mabaharia wote watatu wanamvamia Shume huku Amerigo akimpiga ngumi na mateke kila anapopata nafasi… Mwishowe wanafaulu kumfunga Shume mikono na miguu na kumlaza chini…*) (uk. 31)

Amerigo anakerwa na Shume ambaye anamkosea heshima kwa kukosa kupiga saluti. Shume na mamake wanatazamana ili kuhimizana. Amerigo anazidisha dhuluma dhidi ya Wazanji ili Sudana asalimu amri yake. Mashtaka ya uongo na hukumu kali za kinyama zinatolewa mbele ya Sudana ambaye amefungwa ili kumuudhi. Shume anashambuliwa kwa viboko, mateke na ngumi kwa kuwatusi Wamerope alipoitumia bendera yao kupangusia viatu na kuishusha hadhi yao.

(*Mzanji 4 anasukumwa na kuangushwa mbele ya miguu ya Amerigo.*) (uk. 32)

(*Akimkaripia.*) (uk. 32)

(*Anasitasita huku akimtazama Muzungu.)* (uk. 33)

( *Kwa hasira.*) (uk. 33)

(*Mzanji 4 anakamatwa na Wamerope wawili na wanaanza kumvuruta.*) (uk. 34)

(*Mabaharia na Mzanji 4 wanatoka.*) (uk. 34)

(*Mzanji 5 anasukumwa na kuanguka mbele ya Amerigo.*) (uk. 34)

*(Akimpiga kofi.*) ( uk. 34)

*(Akisimama kwa ghafla)... Anampiga makofi na mateke mpaka anachoka. Huku Mzanji 5 akijaribu kujikinga. Amerigo akiwa anatweta, anarudi kitini na kukaa.*) ( uk. 34)

*(Anajirusha kutoka kitandani akijaribu kumshambulia Amerigo kwa makucha lakini silisili zinamzuia na*

*kumwangusha. Anajaribu kukivuta kitanda lakini anashindwa nguvu…)* ( uk. 35)

(*… akimtazama Sudana.*) (uk. 35)

(*….Na kufunika uso wake kwa mikono yake akijizuilia asilie… Wamerope waliomkamata Mzanji 5 wanapiga Saluti na kutoka nje naye.*) (uk. 35)

Mzanji 4 anahukumiwa viboko ishirini matakoni kwa kufumaniwa akipumzika wakati wa kazi. Hukumu ya Mzanji 5 inabadilishwa kutoka kukatwa mkono hadi kuhasiwa kwa kupatikana akiiba viazi jikoni. Huu ni udhalimu na udunishaji. Jitihada za Sudana mwenye hasira na uchungu za kuwatetea Wazanji wenzake hazifui dafu. Kwa Sudana haya hayavumiliki na ndipo anahisi kichefuchefu. Hii ni ishara ya chuki kwani hakuna mzalendo yeyote anayeweza kuvumilia kushuhudia udhalimu wa aina hii.

(*Sizwe anasukumwa na kuanguka mbele ya Amerigo lakini anajiinua haraka haraka na kusimama tena. Wamerope watatu wanamrukia na kumpigisha magoti kwa nguvu. Wanaendelea kumzuilia asiinuke.*) (uk. 36)

(*Sudana anainua uso na kutazama yanayoendelea kwa hamu.*) (uk. 36)

(*Akisogea mbele.*) (uk. 36)

(*…anamtazama Sudana kwa makini, Sudana naye anamtazama kama anayemwomba amhurumie mtoto wake.*) (uk. 36)

(*Bado akimtazama Sudana.*) (uk. 37)

(*Sudana anashtuka. Ananyosha mkono, mara akimtazama Sizwe mara Amerigo. Anaonekana amefazaika kabisa. Halafu anaanza kulia huku akisukasuka kichwa. Amerigo anatoa ishara Sizwe aondolewe. Mabaharia Wamerope wanamvuta Sizwe na kuanza kutoka naye. Sudana anamtazama…*) (uk. 37)

(*Akiinua mkono.*) (uk. 37)

Sizwe anadunishwa na kulazimishwa kumheshimu na kumsujudia Amerigo kwa kusukumwa na kulazimishwa kupiga magoti. Hii ni baada ya Sudzungu kuwasilisha mashtaka dhidi ya Sizwe. Miondoko hii inamwathiri sana Sudana kwa sababu anayedhulumiwa ni mwanawe. Amerigo anamtazama Sudana kwa makini ili aone hisia zake naye Sudana anamtazama kwa kumsihi asimdhuru mwanawe. Sudana anatishwa na kuhuzunishwa na hukumu ya kifo inayotolewa dhidi ya Sizwe. Haamini kuwa binadamu anaweza kutekeleza udhalimu kama huu na ndipo analia huku akisukasuka kichwa. Sudana anahuzunika kwa kushuhudia mwanawe akimsaliti kaka yake ati kwa kiburi cha kukataa kubomoa mashua ya Zinji ili kuikarabati ile ya Amerope. Mwanawe anayaonea fahari yale ya kigeni.

(…*Sudana anamtazama Amerigo akiwa na tamaa kubwa*)… *Sudana anaendelea kumtazama… halafu anamtazama Sizwe… Anarudi na kumtazama tena Amerigo kwa muda. Anafungua mdomo kama anayetaka kusema jambo.*) (uk.37)

(*Sudana anamtazama tena Sizwe. Anaanza tena kulia kwa*

*nguvu.*) (uk. 37)

*(Wote wanatoka isipokuwa Muzungu.)* (uk. 37)

(*...anasita kidogo, halafu anaondoka akionekana ameudhika. Amerigo anasimama na kumsogelea Sudana. Anajaribu kumgusalakini Sudana anajitupa kando.*) (uk. 37)

(*Kwa hasira)... (Wanatazamana kwa muda, Sudana akiwa na tambo la mnyama mkali aliyeingiwa na hofu.*) ( uk. 37)

(*Akiwa amenuna)... (Anaondoka na kuelekea kwenye mlango. Yuko karibu kutoka.*) (uk. 38)

(*Amerigo anageuka kumtazama Sudana.*) (uk. 38)

(... *Amerigo anarudi polepole pale alipo Sudana.*) (uk. 38)

*(Amerigo anamsogelea, anampapasa nywele na mashavu. Polepole anainuka na kumbusu Sudana... Amerigo anambeba Sudana na kumlaza kitandani. Anavua shati halafu anajilaza kando ya Sudana. Anamkumbatia, akimbusu na kumpapasa huku akijaribu kumvua nguo...*) (uk. 38)

Amerigo sasa amegusa ndipo. Sudana anamtazama Amerigo kuonyesha hamu yake ya kumnusuru mwanawe kisha anamtazama Sizwe akijaribu kusema ametamauka kwani uhai wa mwanawe sasa unategemea uamuzi wake. Sudana anazidi kuhuzunika Sizwe anapomkataza kusalimu amri ya Amerigo. Amegundua kuwa Sizwe amehiyari kifo badala ya mamake kunajisiwa. Amerigo anawauliza wote waliomo chumbani waondoke

ili athibitishe ikiwa Sudana ameshawishika. Muzungu anaudhiwa na hatua hii ambayo inaishusha hadhi yake. Sudana analazimika kumsihi Amerigo amsamehe Sizwe. Hali sasa imekuwa ya nipe nikupe baada ya Sudana kuwekewa masharti. Jambo hili linamfanya Sudana kupandwa na hamaki huku Amerigo akidhani ya kwamba amefaulu. Mwanamke huyu ni kielelezo cha mataifa ya Afrika yaliyolazimika kuumbua utu na hadhi ya watu wake kwa sababu ya vikwazo walivyowekewa na mataifa ya kigeni.

> (*…. Anatazama huku na huku. Amerigo anaonekana haelewi kinachotendeka. Mara Sudana anampiga teke Amerigo na kumwangusha chini. Anakaa kitandani anaziba masikio…)* (uk. 38)
>
> (*Akitweta kwa hasira…*) *Amerigo ananyakua shati lake na kutoka kwa vishindo. Sudana anafunika uso wake… Shume anaingia… Sudana akiinua uso kujipangusa machozi anamwona Shume mbele yake.*) (uk.39)
>
> (*Anamnyoshea mikono. Shume anasogea anapiga magoti na kumkumbatia.*) (uk. 39)
>
> (*Sudana anainua kichwa. Shume anamwacha. Sudana anatazama huku na huku, halafu macho yake yanatua kwa Shume. Anatabasamu kidogo.*) (uk. 40)

Sudana anakanywa na Sizwe kupitia dhamiri yake kukubali najisi. Hisia zake zinamfahamisha kuwa mwanawe tayari ameuawa. Shume anaingia na kumliwaza mamake na kumsihi asilie kilio cha unyonge kwa sababu Sizwe alikufa ili mamake

asinajisike na ili pia damu yake iwe kafara na kinga ya laana. Sizwe ni mfano wa wananchi ambao kila mara huwa tayari kujitolea mhanga. Shume anafahamu kuwa kilio kwa adui ni ishara ya kushindwa na ndipo anamhimiza mamake ajipe matumaini na nguvu.

> (*Amerigo anaingia … mikono nyuma amefuatwa na Wamerope watatu. Mmoja ameshika kamba na kiboko. Wanasimama hatua chache na walipo Sudana na Shume ambao mpaka sasa hawajawaona.*) (uk. 40)
>
> (*…Sudana na Shume wanashtuka. Shume anageuka na kusimama. Amerigo anawasogelea na anasimama mbele yao.*) (uk. 40)
>
> (*Anamgeukia Shume huku uso ameufinya kwa hasira na chuki.*) (uk. 41)
>
> (*Amerigo analeta mkono wake wa kulia mbele na kumwonyesha Shume bunda la noti za Amerope.*) (uk. 41)
>
> (*…..Shume anaitikia kwa kichwa.*) (uk. 41)

Amerigo anaonekana kutambua nguvu na ari ya Sudana na wanawe na ndipo anakuja na Wamerope watatu. Kamba na viboko ni ishara ya udhalimu. Amerigo anakasirishwa sana na kitendo cha Shume cha kuzitusi pesa tukufu za Amerope kwa kuziweka chooni. Sudana anashikwa na wasiwasi kwani anafahamu wazi kuwa mwanawe yuko mashakani. Shume haogopi kumtazama Amerigo kwa ujasiri kwa sababu anajua kuwa baharia huyu anaogopa kukabiliana naye na anawategemea Wamerope wenzake na silaha alizonazo.

> (*…Sudana anamaka kidogo na anaonekana ameingiwa na*

*wasiwasi.*) (uk. 41)

(*Amerigo na Shume wanatazama...*) (*... Wamerope wanamkamata Shume. Shume anapigana nao. Sudana anaingia kati kumsaidia Shume kwa meno na makucha kila anapopata nafasi. Amerigo naye anajaribu kumvuta Sudana. Mabaharia wengine wawili wanakuja kusaidia. Hatimaye Shume anashindwa nguvu. Anafungwa kamba na kubebwa nje. Sudana anamrukia Amerigo akitaka kumtia makucha, lakini silisili inamwangusha...*)

(uk .42)

(*Akisukasuka kichwa.*) (uk 42)

(*Anamsogelea Sudana.*) ( uk. 43)

Shume anahukumiwa viboko kumi mgongoni. Juhudi kubwa zinahitajika kumdhibiti Shume ambaye ana ari kubwa ya kujikomboa. Sudana anajaribu kumshambulia Amerigo kutokana na hasira na uchungu wa wanawe. Anamwambia Amerigo kuwa nguvu na silaha wanazotumia ni dalili kwamba Wamerope wameshindwa kuwatawala Wazanji. Zote ni ishara ya unyonge kwani aliyetawala hahitaji kutenzwa nguvu. Amerigo anashangazwa na usemi huu wa hekima ambao hakutarajia kutoka kwa kiumbe duni kama huyu na anasukasuka kichwa kuonyesha hali ya kuchanganyikiwa. Amerigo anamsogelea Sudana kuonyesha kuwa shauku yake ingali ipo huku akifikiria ya kwamba Sudana ameshawishika kutokana na vitisho na udhalimu wake.

Katika tendo la pili, onyesho la 2:

> (*Kwa hasira*)… (*Amerigo anamrukia Sudana wanabumburushana huku na huku, Amerigo akijaribu kuzichana nguo za Sudana. Kichwa cha Sudana kinajigonga na kitanda. Sudana anaanguka na kuzimia. Amerigo anamtingisha… Amerigo anaingiwa na wasiwasi kidogo; anaweka sikio moja kwenye kifua cha Sudana. Anaketi…*)
> (uk. 44)
>
> (*Akitabasamu kidogo*)… (*Amerigo anasimama, anazunguka huku na huku akifikiria la kufanya. Mara anasimama ghafla. Anageuka na kimtazama Sudana…* ) (uk. 44)
>
> (*Anaanza kuvua nguo huku haraka akimsogelea Sudana kwa hamu kubwa mara Shume anaingia kwa ghafla, Mgongo wazi na umejaa damu. Shume na Amerigo wanatazamana kwa muda. Amerigo haraka anatoa bastola Shume anajaribu kumkimbilia amkamate, lakini Amerigo anafyatua risasi. Shume anajishika bega kwa maumivu na anaanguka chini… Amerigo anaitupa bastola Kando. Anaendelea kuvua nguo huku akimsogelea Sudana….* ) (uk. 44)

Jitihada za Amerigo za kutekeleza maovu zinabainika anapozidisha nguvu za kumbaka Sudana ambaye amedhibitiwa kwa silisili. Amerigo anaonyesha furaha baada ya kugundua kuwa Sudana bado yuko hai. Hatimaye furaha yake inazidi anapogudua kuwa

amerahisishiwa mambo baada ya Sudana kupoteza fahamu. Tamaa na hamu yake inasitishwa na Shume anayeingia ghafla huku mgongo wake uliojaa damu ukiwa wazi ili kudhihirisha udhalimu aliotendewa. Amerigo anatoa bastola baada ya kutazamana na Shume na kung'amua kuwa yumo hatarini. Amerigo baada ya kumjeruhi Shume vibaya anatimiza lengo lake bila woga na kudhihirisha udhalimu wa kuajabiwa.

Katika tendo la tatu, onyesho la 1:

*(Mzanji 6 anaingia haraka.)* (uk. 45)

Mhusika huyu amekuja kuwatahadharisha Shume na Wazanji wenzake kuhusu kuja kwa Amerigo. Shume alikuwa akiwaeleza hatua watakazochukua ili idadi ya walionajisika isiongezeke kwani itaendelea kuwasaliti.

(*Haraka haraka Shume anajilaza kitandani na kufumba macho. Wenzake wanamzingira na kuanza kuomboleza. Amerigo anaingia huku amefuatwa na Sudzungu. Wazanji waacha kuomboleza, Wanampigia saluti Amerigo na kusimama kando ya chumba. Amerigo anakikaribia kitanda alicholalia Shume. Anamtazama Shume, halafu anawatazama Wenzake.*) (uk. 45)

(*Kwa ukali.*) ( uk. 45)

(*Amerigo anageuka na kuanza kutoka, Sudzungu nyuma yake.)* (uk. 45)

(... *na kumtazama.*) (uk.46)

*(Akitabasamu kidogo.)* (uk. 46)

(*Anaanza tena kutoka.)* (uk. 46)

(... *na kugeuka tena, akionekana amekereka kidogo.*)

(uk. 46)

(*Amerigo anafikiri kidogo halafu anamtazama Sudzungu. Sudzungu anaitikia kwa kichwa.*) (uk. 46)

*(Akiitikia kwa kichwa)... (Wazanji wanaonekana wamefurahi na wanampigia Amerigo Saluti. Amerigo na Sudzungu wanatoka. Wazanji wanamzingira tena Shume na kuendelea kuomboleza. Sudana anaingia huku analia... Sudana anamwona Shume kitandani...Anamsogelea Shume pole pole mkono mbele tayari kumkumbatia mara Shume anajiinua na kusimama ... Sudana anamaka huku anaendelea kulia. Shume anamsogelea. Wanakumbatia... Shume anawacha kumkumbatia Sudana. Anamshika mkono, Shume na Sudana wanatazama.*) (uk. 47)

Shume katika kujilaza kitandani na kufumba macho huku Wazanji wenzake wakiomboleza ni mbinu ya kumpotosha Amerigo pamoja na kikaragosi wake Sudzungu kuhusu hali ya Shume. Wazanji wanampigia Amerigo saluti kuonyesha heshima bandia za kumpumbaza. Amerigo anawatazama Wazanji baada ya kumtazama Shume ili aone hisia zao. Amerigo anatabasamu kwa furaha baada ya kufahamishwa na Mzanji 6 kuhusu nia ya Shume ya kutaka kuomba msamaha baada ya yeye kujuta kwa kumkosea heshima. Amerigo anakerwa na Mzanji huyu ambaye anamsimamisha tena ili kumsihi awaruhusu Wazanji wampigie na kumchezea ngoma ya toba kwa niaba ya Shume. Wazanji wamezindua mbinu mpya ya kukabiliana na adui kwani matatizo yanapokithiri

watu hawana budi kupanga mikakati ya kujinasua. Amerigo anamtazama Sudzungu ili apate hakikisho kuhusu ngoma hii naye Sudzungu anamhakikishia kwa ishara ya kichwa. Wazanji wanafurahishwa na kibali hiki na wanampigia Amerigo saluti kama ishara ya heshima. Wazanji wanamzingira Shume ili asionekane huku wakisikiliza ushauri wake kuhusu hatua watakazochukua ili idadi ya walionajisika isiongezeke na kuendelea kuwasaliti. Sudana anamsogelea Shume polepole huku akiwa tayari kumkumbatia kwa huzuni huku akifikiria kuwa mwanawe amekufa.

> (*Kwa masikitiko*)... *(Sudana anaitikia kwa kichwa. Shume anamkumbatia tena. Halafu anamshika mkono mmoja na kuanza kutoka naye.... Wote wanatoka... Mwanamke kisu mkononi anaingia akifuatwa na msichana. Wanaelekeana na wanaanza ...*) (uk. 47)
>
> (*...Mwanamke, kisu akikichezesha kama ambaye yu tayari kuchinja. Anamsogelea msichana. Anapofika karibu anakiinua tayari kumchoma nacho...*) (uk. 50)

Shume anamshawishi mamake atakaswe na najisi iliyompata ili isiwaathiri. Sudana anaonyesha ishara ya kukubali jambo ambalo linamfurahisha Shume ambaye anapendezwa na uamuzi huu wa kijasiri. kisu kinachoinuliwa tayari kumchinja msichana ni tambiko la kumtakasa Sudana kutokana na najisi.

Tendo la tatu, onyesho la 2:

> (*Akitazama huku na huku.*) (uk. 51)
>
> (*Shume anasogea mbele kidogo.*) (uk. 51)

*(Shume anarudi mahali pake anatoa ishara kwa mikono. Wazanji wote isipokuwa wapiga ngoma wapiga safu mbili. Shume anatoa tena ishara. Ngoma zinaanza tena na wote wanaanza kucheza pamoja na Sudana... Shume anarusha upanga wake huku na huku. Baada ya muda Shume anapiga makofi na ngoma na wachezaji wanasimama. Wamerope Wanawapigia makofi. Shume anasogea mbele kidogo.)*

( uk. 52)

*(Amerigo anaitikia kwa kichwa. Shume anapiga makofi mara mbili. Mzanji mmoja anaingia huku amebeba boksi. Anakwenda na kuliweka boksi mbele yao. Halafu anasimama, anapiga saluti na anaondoka. Muzungu anasimama kulifungua boksi huku Shume akisongea mbele alikokaa Amerigo. Muzungu analifungua boksi. Muzungu na Amerigo wanainama kuchungulia ndani...)* (uk.52)

Amerigo anatazama huku na huku kwa hofu na wasiwasi baada ya kukosa kumwona kikaragosi wake Sudzungu wakati wa ngoma. Amerigo bado anamshuku Shume hasa kwa kutozifahamu ishara zinazotumiwa katika ngoma hii. Shume anawaeleza makaburu matokeo ya ngoma. Ni ngoma ya mauti ya kuua chuki. Ngoma inapokamilika kwa amani Amerigo anaonyesha ishara ya kukubali msamaha. Shume anapiga makofi mara mbili ili kumkaribisha Mzanji anayekileta kichwa cha Sudzungu kwenye boksi kama mkono wa wa kutubia.

*(Wote wawili wanajirusha nyuma, kila mmoja akianguka*

*upande wake. Halafu vurumai linaanza jukwaani, Wamerope wakigongana, wengine wakijaribu kuwasaidia Amerigo na Muzungu wengine wakianza kupigana na Wazanji. Katika vurumai hii, Shume anajirusha na upanga wake na yuko tayari kumkata Amerigo kichwa lakini Muzungu anawahi kuchomoa na kufyatua bastola yake. Shume anaanguka… Kila mmoja anamtazama Shume, Shume anajaribu kujiinua, upanga bado mkononi, damu zinaonekana zikitoka kifuani mwake… Amerigo naye anachomoa bastola yake… Anamlenga Shume na anaifyatua risasi Shume anaanguka tena… Shume anainua kichwa kidogo.*) (uk. 53)

Shume anapata nafasi ya kuwaonya Amerigo na Muzungu kuwa wakati ungali pamoja nao.

> …(*Amerigo na Muzungu wanafyatua tena bastola zao kwa pamoja, kichwa cha Shume kinaanguka. … Halafu anamkimbilia Shume anakaa chini, anamgeuza na kukiweka kichwa chake mapajani mwake huku akitokwa na machozi. Hasira usoni na mikono yao imekunja ngumi. Wazanji… Huku wakisogelea Amerigo , Muzungu na Wamerope wengine , Wamerope wanaonekana wameingiwa na hofu. Amerigo na Muzungu wanawaelekeza Wazanji bastola zao. Lakini bado wazanji wanasogelea tu. Amerigo,*

*Muzungu na Wamerope wengine wanaanza kurudi kinyumenyume, polepole mpaka wote wanatoka wakifuatwa na Wazanji...anainua mkono wa kulia huku amekunja ngumi.*)

(uk. 53)

(*Anainua ngumi.*) ( uk. 53)

Maelekezo haya kuhusu miondoko yanaonyesha nguvu na ari ya kujikomboa kwa damu na roho. Vurugu linaanza baada ya makaburu kukiona kichwa cha Sudzungu ndani ya boksi lililoletwa kama mkono wa kutubia. Amerigo na Muzungu wanajirusha nyuma kwa hofu baada ya kuchungulia ndani ya boksi. Shume anaanguka baada ya kupigwa risasi katika vurugu lakini anajaribu kujiinua upanga ukiwa bado mkononi kama njia ya kuwahimiza wazanji wenzake wasikate tamaa ya kujikomboa. Huzuni na mapenzi ya Sudana kwa mwanawe yanabainika anapougeuza mwili wa Shume na kukiweka kichwa chake mapajani mwake. Hatua ya Wamerope kurudi kinyumenyume kwa hofu na silaha zao mikononi huku wazanji wakiwasogelea ni ishara kuwa ari, ushirikiano na ujasiri wa Wazanji ni msukumo wa kuwapa ushindi. Mwisho unadhihirisha matumaini kwa sababu Wazanji hawaonyeshi ishara ya kutishwa au kurudi nyuma. Wametambua ukweli kwamba, umwagikaji wa damu hauwezi kuepukika katika harakati za ukombozi. Sudana anainua ngumi ili kuwahimiza Wazanji waendelee na mapambano kwa ujasiri.

Mazrui na Njogu wamekitumia kipengele hiki cha miondoko kwa ubunifu na upana katika kusaidia kupatikana kwa maana ya matini. Maelekezo marefu ya jukwaa kuhusu miondoko yamechukua nafasi kubwa katika tamthilia kulingana na majukumu. Ishara za

viungo vya mwili na uso zimehusika katika kutoa hisia za ndani na hata kuonyesha misimamo. Miondoko katika tamthilia hii imekuwa na athari kubwa katika kustawisha ujumbe wa watunzi. Wasifu na saikolojia ya wahusika imebainika kupitia utendaji wao.

### 4.1.4 Uangazaji

Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele hiki ambacho huongeza umuhimu katika utendaji.

Katika utangulizi:

(… *Taa zinazima…*) (uk. 6)

Hii ni baada ya mhusika Sudana kukamilisha masimulizi yake katika utangulizi. Hali hii inazua taharuki baada ya Sudana kusema na kuwaombea wanawe na kisha kusema kuwa wakati, bila shaka uko upande wao katika mapambano ya ukombozi.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 1:

(…*Amerigo amejifunga kitambaa chekundu*…) (uk. 9)

Rangi hii inaangazia hatari aliyobeba nahodha huyu wa Wamerope. Yeye na mwenzake wamejifunga panga na bastola kiunoni. Wanawanasa wazanji kwa hila na kisha kuwafanya watumwa.

(*Taa zinazima*) (uk. 15)

Hii ni baada ya Mashua ya ZINJI kufungashwa na ile ya AMEROPE, naye Amerigo kumtazama Sudana kwa jicho la matamanio. Taa kuzimika ni ishara ya uovu. Wazanji wamenaswa kwenye mtego na sasa wao ni mateka wa kuwatumikia makaburu. Huu ni mwanzo wa masaibu ya Sudana kwa sababu ya jinsia yake.

(*Taa zinazima.*) (uk.21)

(... *Taa inazima...*) (uk. 31)

Hapa ni baada ya Shume kupinga kuvunjwa mashua ya ZINJI ili kuitengeneza mashua ya AMEROPE. Amerigo anamshuku mhusika huyu kwa kuwa hii ni dalili ya kuzinduka na kuwa pingamizi katika harakati za makaburu kukusanya watumwa. Ukweli unabainika Shume anapoitusi na kuidharau bendera ya makaburu kwa kuipangusia viatu na kisha kuadhibiwa kwa michapo ya kiboko.

Katika tendo la pili, onyesho la 2:

(*Taa zinazima*) (uk. 44)

Hali hii inaashiria maovu wanayotendewa Wazanji. Mzanji 4 anahukumiwa viboko ishirini matakoni, adhabu ya Mzanji 5 inabadilishwa kutoka kukatwa mkono hadi kuhasiwa. Sizwe ananyongwa huku Sudana ananajisiwa.

(...*Mwangaza unapungua...* ) ( uk. 49)

Shume anamuuliza mamake akubali kutakaswa najisi. Ufifiaji wa mwangaza unaashiria hali ya kutokuwa na hakika kwa sababu hiki ni kitendo cha kujitolea mhanga. Sudana hana hakika ikiwa atavumilia maumivu. Naye Shume hajui ikiwa mamake atakubali tambiko hili lenye maumivu na linalohitaji ujasiri.

Tendo la tatu, onyesho la 1:

(... *Taa zinazima..*) (uk. 50)

Hali hii inatokea wakati Mwanamke anapokiinua kisu tayari kumchoma msichana ili asizae kizazi kitakachomgeukia.

(... *Taa zinazimwa.*) (uk. 54)

Jambo hili linatendeka mwisho wa mchezo wakati Sudana akiendelea kusema, mapambano yanaendelea huku akijibiwa na sauti nyingine. Hali hii inazua taharuki kwa sababu Wazanji wanaendelea kuwasogelea Wamerope bila kuogopa bastola. Haya ni mapambano kati ya walio na silaha kali na walio na ari na ujasiri.

Uangazaji umetumika kuzua mazaji na kuyafungamanisha na ujumbe wa tamthilia. Giza limetumikaa kama fumbo la maovu yanayotendeka kindanindani. uangazaji pia umetumika ili kuiwezesha hadhira kuona yale yanayotendeka katika jukwaa.

### 4.1.5 Sauti

Kipengele hiki cha utendaji ambacho kinasikika badala ya kuonekana kimechunguzwa katika tamthilia ya *Sudana.*

Katika utangulizi:

(*... Mdundo wa ngoma unasikika kwa mbali.*) (uk. 1)

Sauti hii inasikika katika sehemu ya utangulizi wakati wa masimulizi ya Sudana kwa hadhira. Ngoma ni muhimu katika utamaduni wa Mwafrika kwa sababu ya kuwasilisha ujumbe unaofahamika na jamii husika.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 1:

....(*Anacheka kidogo)... (Anacheka tena kidogo...) ...(Anacheka... anapiga mbinja pole pole, halafu wote wanaanza kuimba.*) (uk. 8)

Mzanji 3 katika mashua ya Amerope anacheka baada ya Mzanji 1 kusema kuwa wasiipoteze tamaa ya ukombozi. Kwake yeye hiyo ndiyo hatima yao. Katika wimbo, Wazanji wanakumbuka walivyotekwa nyara na maharamia, mateso wanayopitia huku

wakijipa matumaini ya ukombozi. Wimbo unawapa ari ya kufanya kazi na pia kuwaunganisha.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 2:

(… *Huku wanaimba…*) (uk. 16)

(*Sauti za Wazanji zinapaa katika wimbo …*) ( uk. 18)

(*Huku akicheka*)… *Amerigo naye anacheka kidogo)…*

(*Wanacheka tena.*) (uk. 18)

…(*Anacheka tena kidogo)…(Anacheka kidogo*)…

(*Kicheko kinazidi… Muzungu naye anaanza kucheka punde si punde, nao pia wanaanza kucheka…*) (uk. 18)

Amerigo na Muzungu hawajui ni kwa nini Wazanji wanacheka nao Wazanji hawajui kwa nini Amerigo na Muzungu wanacheka. Kuna shaka kati ya vikundi hivi viwili.

(…*Wanaanza kucheka tena lakini sasa polepole.* ) (uk .19)

(…*Huko ndani tunasikia ghasia. Amri zikitolewa, mbao zikakatwa na zingine zikivunjwa na milio ya misumeno, nyundo na misumari*) (uk. 21)

Vicheko vya Amerigo na Muzungu ni katika kuwakejeli Wazanji wanaoimba kwani ngoma ndicho kitu cha pekee walichorithi kutoka kwa Mungu huku Wamerope wakirithi hekima. Hili ni dhihirisho la utamaduni wa Mwafrika kudunishwa na kuonekana kama upumbavu mbele ya makaburu. Harakati za kuivunja mashua ya ZINJI zinaashiria kuumbuliwa kwa amali za Mwafrika.

Katika tendo la pili, onyesho la 1:

(*Wanasikia sauti ya Amerigo akiimba*) ( uk. 23)

(*Akicheka.*) (uk. 23)

(... *anapiga siyahi...*) ( uk. 25)

(... *Mlango unabishwa.*) (uk. 28)

Katika tendo la pili, onyesho la 1:

(...*anatoa sauti kama anayetaka kutapika...*) (uk. 35)

Amerigo anaimba na kucheka kwa furaha baada ya kufaulu kumtumia Sudzungu kutekeleza haja yake ya kumshawishi Sudana lakini furaha yake inafika kikomo anapoumwa shingoni na Sudana. Ukatili wa Amerigo kwa Wazanji unamfanya Sudana kujawa na chuki kiasi cha kuhisi kutapika. Amerigo anaamua kumdhibiti mwanamke huyu ambaye amedhihirisha ujasiri wake.

(... *halafu anaanza kulia... kilio kinazidi.*) (uk. 37)

(...*Anaanza tena kulia kwa nguvu.*) (uk. 37)

(...*Anaendelea kulia....*)...*(Sudana anazidisha kilio kidogo... mara ghafla Sudana anasikia sauti zikitoka kila upande.* ) ( uk. 38)

(... *Anaendelea kulia pole pole.*) (uk. 39).

(*Amerigo anacheka kwa kejeli.*) (uk. 40)

(*Akiendelea kucheka polepole.*) (uk. 40)

(*Akicheka kwa kejeli.*) (uk. 41)

Sudana analia kwa huzuni baada ya Amerigo kutoa hukumu ya kifo kwa Sizwe. uchungu wa uzazi unamlazimisha kukata tamaa ya kuhifadhi hadhi yake lakini dhamiri yake kupitia mwangwi wa sauti ya Sizwe kutoka kila upande zinamkanya dhidi ya kunajisiwa

kwa hiari kwa sababu yeye amejitolea kufa ili mamake asinajisike. Amerigo anacheka kwa kejeli anapomsikia Sudana akizungumza na Sizwe ambaye tayari ni mfu huku akimhakikishia kuwa hatakufa kwa sababu katika kifo chake mna mbegu zisizo idadi. Damu ya Sizwe itaipalilia ari ya Wazanji ya kujikomboa. Amerigo haelewi ujumbe huu na anauchukulia kama ujinga kwa sababu hajui ya kwamba Waafrika huishi hata baada ya kifo.

Katika tendo la tatu, onyesho la 1:

> (… *Wazanji wanaanza kuomboleza…*) (uk. 45)
>
> (… *Maumivu ya Sudana yanaendelea kusikika mara kwa mara)* (uk. 47)

Katika tendo la tatu onyesho la 2:

> (… *Wanapiga kelele)* (uk. 52.)

Amerigo na Muzungu wameshtuka na kuogopa baada ya kukiona kichwa cha Sudzungu kwenye boksi.

> (…*Sudana anapiga makelele…Wazanji wanaanza kuimba…*) (uk.53)

**SAUTI**

**NYINGINE:** (Kwa ndani) Mapambano yaendelee!

**SAUTI:** Mapambano yaendelee!

Maombolezi bandia ya Wazanji yananuia kumpotosha Amerigo kuhusu hali ya Shume. Wazanji sasa wameibuka na mbinu mpya za kukabiliana na adui. Sauti za maumivu zinabainisha uchungu unaotokana na kutakaswa kwa Sudana. Amerigo na Muzungu

wanapigwa na butwaa na wanapiga kelele baada ya kukiona kichwa cha Sudzungu kwenye boksi. Sudana anapiga makelele kwa uchungu na huzuni baada ya kumpoteza Shume mwanawe aliyekuwa amesalia katika mapigano. Sudana anajiunga na Wazanji wenzake katika kuimba kama ishara ya kuendeleza mapambano ya ukombozi kwa ushirikiano. Watunzi wa tamthilia kwa kutumia kipengele hiki kwa ustadi wamebuni sauti zinazodaiwa na matini ili kufanikisha ujumbe. Wametumia kicheko, sauti ya ngoma, nyimbo, siyahi, na kilio ili kuwawezesha waigizaji kuuwasilisha ujumbe kwenye jukwaa.

### 4.1.6. Kimya

Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele hiki cha utendaji ambacho hakishughulishi macho na masikio.

Katika tendo la kwanza, onyesho la 1:

… (*Kimya* …) (uk. 8)

Hali ya Wazanji waliokuwa wakiimba baada ya kunyamazishwa na Muzungu.

Katika tendo la kwanza, onyesho 2

(…*Kimya kidogo*) (uk. 17)

(*Kimya*…) (uk. 20)

(*Kimya*) (uk. 20)

Kimya kinatokea baada ya Mzanji 3 kuwaza juu ya ushauri wa Mzanji 1 kwamba wasiitupe tamaa ya ukombozi ili nayo tamaa isiwatupe. Kwake yeye haelewi kwa sababu hali yao ni ya kutamausha. Wazanji wananyamaza baada ya Amerigo na Muzungu kuingia kwa sababu wimbo wao una ujumbe wa kuhimizana ambao hawangependa makaburu hawa wausikie. Kimya kinatokea tena wakati Amerigo

anamweleza Muzungu asili ya umuhimu wa ngoma na nyimbo miongoni mwa Wazanji kulingana na mafunzo waliopata katika madarasa ya dini wakiwa wachanga. Mungu baada maumbaji aliyaita makabila yote kwa zamu ili waombe walichotaka. Kabila la Wamerope lililoitwa mwanzo liliomba hekima huku Wazanji waliokuwa wa mwisho kuitwa wakapewa ngoma kwa sababu ndicho kitu cha pekee kilichobaki. Makaburu hawa bila shaka walisahau umuhimu wa ngoma hii kwa kuwa ndiyo iliyotumiwa na Mungu kuwaita watu wa makabila yote. Hii ndio asili ya makaburu kumchukulia Mwafrika kama mtu mjinga asiyekuwa na hadhi yoyote. Kimya pia kinatokea baada ya Mzanji 4 kuleta habari za mbao kuoza na maji kuanza kuingia chomboni. Mzanji huyu ambaye ana hofu ananyamazishwa na Muzungu. Muzungu na Amerigo tayari wana suluhisho. Tangu awali walijua kuwa mashua waliookoa ni akiba ya mbao.

Katika. tendo la pili, onyesho la 1:

(*Kimya.*) (uk. 24)

Kimya hiki kinatokea baada ya Amerigo kumtusi na kumfukuza baharia Mwamerope aliyeingia chumbani mwake bila kubisha na kusitisha juhudi zake za kumnajisi Sudana. Amerigo anasema mabaharia wengine hawakufundishwa adabu za kimsingi. Hiki ni kinaya kwa sababu mtovu wa adabu na maadili ni yeye.

(*Kimya* ) (uk. 25)

Hii ni baada ya Sudana kumpiga meno shingoni huku Amerigo akisema kuwa anajua ni papatiko la mapenzi. Tamaa imempofusha kiasi cha kutouona ukweli kwamba Sudana anamchukia.

(*Kimya )* (uk. 28)

(*Kimya* ) (uk.. 29)

(*Kimya*)... *(Kimya*) ( uk. 30)

Katika tendo la pili, onyesho la 2:

(*Kimya*.... ) (uk.36)

Kimya hiki kinatokea baada ya Sudzungu kumsaliti ndugu yake Sizwe na kusababisha kunyongwa kwake. Hili bila shaka ni jambo la kuatua moyo.

(Kimya ) (uk. 38)

Amerigo anapompa Sudana masharti ya akubali kushiriki mapenzi naye au Sizwe anyongwe. Ufuska kubadilishwa na maisha ni jambo la kusikitisha.

(...*anaingia kimya kimya.*) (uk. 39)

Katika sehemu hii kimya kinatokea na kupisha nafasi ya kuwazia ujumbe. Shume anaingia aliko mamake katika hali hii ya kimya. Amebeba ujumbe wenye huzuni kubwa kuhusu kifo cha kakake Sizwe.

(*Kimya*...) (uk. 41)

(*Kimya*) ... *(Kimya.*) (uk. 43)

. (*Kimya*) (uk. 44)

Kimya katika sehemu hii kinatokea kabla ya Amerigo kumhukumu Shume kwa kosa la kuzikashifu pesa tukufu za Amerope kwa kuziweka chooni jambo ambalo linabainisha ujasiri wa Shume. Kimya kinatokea wakati Amerigo anashindwa kufasiri maneno ya Sudana anayemwambia kuwa kuwanyima uhuru na kuwaumbua ni dalili ya kushindwa kuwatawala. Kimya kinatokea baada ya Sudana kupoteza fahamu na Amerigo kumpiga Shume risasi begani na kisha anaendelea na harakati zake za kumbaka Sudana. Huu ni

udhalimu uliokithiri na ambao hauvumiliki. Wazanji sasa wamo kwenye hatari ya kuangamia. Hawana budi kuchukua hatua ya dharura kwa kufanya tambiko ili najisi isiwaangamize.

Katika tendo la tatu, onyesho la 1:

(... *Kimya.*) (uk. 47)

( *Halafu kimya.*) ( uk. 50)

(...*Kimya*) (uk. 53)

Katika tendo la tatu onyesho la 2:

(... *Kimya...*) ( uk. 53)

( *Kimya...*) (uk. 54)

Kimya kinachotokea katika sehemu hii kinatoa nafasi mwafaka ya kuuwazia ujumbe. Amerigo anawaruhusu Wazanji kumuomba msamaha kwa niaba ya Shume kupitia ngoma ya toba. Kinaya hapa ni kwamba anayestahili msamaha ni Shume aliyejeruhiwa kwa kupigwa risasi. Kimya pia kinatokea baada ya tambiko la kumtakasa Sudana. Hili ni tukio muhimu sana miongoni mwa Wazanji kwa sababu litawaepusha na maangamizi. Kimya kinatokea wakati wa mapigano ambapo Wamerope wanarudi kinyumenyume huku Wazanji wakiwasogelea. Hii ni ishara ya ushindi kwa Wazanji ambao silaha yao ni ari, ujasiri na ushirikiano. Kimya kinachotokea mwisho wa mchezo kabla ya taa kuzima kinaipa hadhira nafasi ya kuwaza. Ukweli kwamba wakati uko upande wa Wazanji umedhihirika kama walivyohakikishiwa na Sudana katika utangulizi. Kipengele cha kimya kimetumiwa katika tamthilia kusisitiza ujumbe maalum na kuuweka mbele ili uweze kuwaziwa kwa makini.

### 4.1.7 Mihimili

Katika sehemu hii tunatathmini ikiwa Mazrui na Njogu wamefanikiwa kutumia mihimili au visaidizi ili kufanikisha utendaji wa tamthilia ya *Sudana* kwenye jukwaa. Katika tendo la kwanza, onyesho 1:

(*...Wakitia tanga, viraka, nyavu , makasia, nanga na ala nyingine za kibaharia...*) (uk. 7)

Visaidizi hivi vinaonekana dekini ili kuthibitisha kuwa uigizaji unatokea baharini.

Katika onyesho la pili:

(*...anatoa Kijaluba cha tumbaku...*). (uk.10)

Kifaa hiki kinabainisha kuwa mhusika Amerigo ni mraibu wa tumbaku.

(*...Wanavutwa kwenye jukwaa kwa kamba...*) (uk.12)

Kamba inadhihirisha kuokolewa kwa Wazanji na kuingia kifungoni bila kujua. Itawabidi kuwatumikia Wamerope daima.

Tendo la pili, onyesho la 1:

(*...Sudana amekaa kitandani...* (uk. 22)

Kitanda ni kifaa ambacho kinatuelekeza kwenye wasifu wa Amerigo pia kinatuashiria dhuluma za Amerigo na usaliti wa Sudzungu ambaye yuko katika chumba cha Amerigo kama gawadi wa mamake. Kifaa hiki kimekuwa kama laana kwa Sudana.

(*...Anauchomoa upanga ...)* (uk.27)

(*...Wamerope wawili ambao wamebeba silisili...*) ( uk.28)

Vifaa hivi ni ishara ya udhalimu kwa sababu Amerigo anavitumia kumtisha na kumdhibiti Sudana baada ya kugundua ujasiri wake. Hali hii inarejelewa katika onyesho la pili.

(*Sudana bado yupo kitandani amefungwa silisili …*) (uk. 32)

(*…Halafu Shume anachukua viatu, anatoa kitambaa kikubwa kutoka kabatini…*(uk. 29)

Vifaa hivi, viatu, kitambaa na kabati vinasaidia kudhihirisha ujumbe wa mtunzi. Udunishaji unabainika Shume anapoamrishwa kuvipangusa viatu vya Amerigo. Shume anachukua nafasi hii kuwadunisha Wamerope Kwa kuitumia bendera yao kupangusia viatu. Adhabu ya viboko inayotolewa inamdunisha Shume na Wazanji wenzake kwa sababu hata Mzanji 4 aliyepatikana akipumzika wakati wa kazi aliadhibiwa kwa kiboko.

Katika tendo la pili, onyesho la 2 :

(*Na kumwonyesha Shume bunda la noti za Amerope…*)

(uk.41)

Bunda hili la noti linazidi kudhihirisha jinsi Shume alivyokuwa na ujasiri wa kupinga dhuluma za Wamerope dhidi ya Wazanji. Anamwekea Amerigo pesa hizi chooni kama karatasi za kujipangusia. Matokeo ni dhuluma zaidi kwa kufungwa na kuchapwa.

(*…Mwanamke kisu mkononi…*) (uk.47)

Kisu hiki kinachangia uwelewa wa yale yanayoonekana kwenye jukwaa kama wanavyoeleza Griffiths na Hemming (1984) kwa vile ndicho kinatumika kuondoa najisi miongoni mwa Wazanji kwa kumtakasa Sudana.

(*...wameketi vitini... Pamoja na Ngoma na Marimba*

*yao. Shume ameshika upanga mkononi.* (uk.51)

Vifaa katika maelekezo haya vinasaidia kuweka wazi wazo la mwandishi. Amerigo na Muzungu wametulia kwenye viti hivi wakisubiri Shume atubu na aombe msamaha kupitia ngoma ya toba. Hiki ni kinaya kwa sababu Shume ndiye amedhulumiwa.

(*... Huku amebeba boksi*)

Hili boksi limebeba kichwa cha Sudzungu ambacho kimeletwa mbele ya Amerigo na Muzungu kama onyo kwao. Sudzungu kwa kuwasaliti Wazanji ameuawa kama njia ya wao kujitakasa. Hii ni ishara kwamba Amerigo na wenzake pia wamo hatarini.

Visaidizi vimetumika katika tamthilia hii ya *Sudana* kuwawezasha waigizaji kuigiza nafasi za wahusika na kuwasilisha ujumbe wa watunzi kwenye jukwaa.

## 4.2 Hitimisho

Katika sura hii tumevitathmini vipengele vinavyofanikisha utendaji katika tamthilia ya *Sudana*. Vipengele hivi ni mandhari, maleba, miondoko, uangazaji, sauti, kimya na mihimili. Sura ya tano na ya mwisho imeshughulikiwa muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tunawasilisha tamati ya utafiti wetu. Tumetathmini utendaji katika tamthilia mbili za Kiswahili. Katika kutimiza lengo letu la utafiti, tumewasilisha tasnifu hii katika sura tano. Mambo tuliyoyashughulikia ni haya; sura ya kwanza ni somo la utafiti. Sura ya pili ni ufafanuzi wa vipengele vinavyochochea na kufanikisha uigizaji wa tamthilia kwenye jukwaa. Katika sura ya tatu tumetathmini vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Kimya kimya kimya*. Katika sura ya nne tumetathmini vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Sudana.* Utafiti wetu umebainisha jinsi vipengele hivi vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia kwenye jukwaa. Sura ya tano ni muhtasari wa matokeo ya utafiti na mapendekezo.

## 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Kwa msingi wa madhumuni na nadharia yetu, imebainika katika utafiti wetu kuwa katika kuangazia vipengele vya utendaji huna budi kugusia namna vinachangia na kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia jukwaani na kuusukuma mchezo mbele. Tumetaja kwa ufupi ujumbe ambao umefungamana na vipengele vya utendaji suala ambalo linakubaliana na maoni ya Williams (1968) ya umuhimu wa kuchunguza uhusiano uliopo kati ya matini na utendaji. Tumebainisha ya kwamba tendo la kidrama hufungamana na usemi wa kidrama. Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* na ya *Sudana* zinaweza kudai nafasi kama matini za kidrama. Hii ni kwa sababu katika kuzitathmini tamthilia hizi tulibaini ya kuwa watunzi wake wamevitumia vipengele vya utendaji hata ingawa

viwango vya matumizi vinatofautiana. Katika tamthilia hizi mbili, maelekezo ya jukwaa yamebuniwa kulingana na mahitaji ya uigizaji na kuusogeza mchezo mbele.

Katika sura ya kwanza, tuliibua maswali mawili ambayo utafiti wetu ulinuia kuyajibu. Kutokana na utafiti huu, hatuna budi kusema kuwa maswali yetu yamejibiwa. Awali, tulijiiuliza ni vipengele vipi vinavyofanikisha utendaji katika jukwaa vilivyotumiwa na watunzi wa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* na ya *Sudana.* Pili, tulijiuliza ikiwa watunzi wa tamthilia hizi mbili wamefanikiwa katika kuwasilisha tamthilia ambazo zinaweza kudai nafasi kama matini za kidrama. Haya yamedhihirika katika utafiti huu kwa sababu stadi zinazofanikisha uigizaji kwenye jukwaa zimetumika katika tamthilia hizi.

Sura ya pili, imeviangazia vipengele vya utendaji kwa kuvifafanua na kuvitolea mifano. Katika kazi hii tumefafanua umuhimu wa kila kipengele katika kudhihirisha matendo ya wahusika na mambo yanayoonekana katika jukwaa ili kuipa tamthilia uhai.

Katika sura ya tatu tumetathmini uwepo wa vipengele vya utendaji katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya.* Utafiti wetu umeonyesha kuwa Mohamed amefanikiwa katika kuwasilisha matini ya kidrama. Hii ni kwa sababu amefanikiwa kuvihusisha vipengele vinavyowawezesha waigizaji kuwasilisha ujumbe kwenye jukwaa. Vipengele hivi ni: maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, uangazaji, miondoko, sauti, kimya na mhimili.

Katika sura ya nne tumeitathmini tamthilia ya *Sudana.* Utafiti umedhihirisha ya kuwa *Sudana*, inaweza kudai nafasi kama tamthilia kwa kuvitumia vipengele vinavyofanikisha

uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa. Katika tamthilia hizi mbili, kipengele cha miondoko kimetumika zaidi ikilinganishwa na vipengele vya maleba, uangazaji, mandhari, sauti, kimya na mihimili. Jambo lingine ambalo limebainika katika utafiti huu ni kuwa vifuasi vya maleba kama vile vipodozi na mafigu havikutumika kamwe. Hivyo basi ni bayana kuwa watunzi wa tamthilia huwatarajia waongozaji wa tamthilia pamoja na waigizaji wao wawe na kipawa na uzoefu wa kubuni mambo ambayo yatafanikisha utendaji kwenye jukwaa.

## 5.2 Hitimisho

Nia yetu katika utafiti huu ilikuwa ni kuviorodhesha na kuvifanua vipengele vinavyofanikisha utendaji katika matini za kidrama. Tulinuia pia kutathmini tamthilia mbili za Kiswahili kwa msingi wa madhumuni yetu. Katika kazi yetu tumethibitisha ya kwamba tamthilia ya *Sudana* na ya *Kimya Kimya Kimya* zinaweza kudai nafasi kama matini za kidrama. Hii ni kutokana na ufanisi wa watunzi wa tamthilia hizi mbili katika kuvitumia vipengele vinavyowawezesha waigizaji kupitisha ujumbe wa matini kupitia uigizaji kwenye jukwaa.

## 5.3. Mapendekezo

Baada ya kuizingatia kazi hii, tumegundua kwamba kuna mengi ambayo yanaweza kuchunguzwa katika tamthilia za *Sudana* na *Kimya Kimya Kimya*. Utafiti wa baadaye unaweza kuchanganua taswira ya mwanamke, ubabedume, fani na mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko ya jamii. Kwa utafiti wa siku zijazo katika matini za kidrama, tunapendekeza utafiti ufanywe kuhusu mandhari halisi na yasiyo halisi kwa sababu hii ni

dhana pana ambayo inaweza kufasiriwa kwa njia anuwai kutegemea mkabala wa mhakiki. Lugha ya kidrama pia ni jambo ambalo tungependa lishughulikiwe kwa sababu ya umuhimu wake katika kufanikisha utendaji kwenye jukwaa. Nadharia hii ya utendaji inaweza pia kutumiwa katika kuzitathmini tamthilia za watunzi wengine.

## MAREJELEO


Arege, T. M. (2009) *Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Oxford University Press.

_________________ (2011) *Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide- Muwa.

Aston, E. & Savona, G. (1991) *Theatre as Sign System*. London & New York: Routledge.

Auslander, P. (2008) *Theory for Performance Studies. A students guide*. London and New York: Roughtledge. www.mohamedrabeea.com

Butler, J. M. (1975) *Drama Projects for Secondary Schools*. Australia: Pergamon Press Ltd.

Griffiths, M. & Hemming, E. (1984) *A Sense of Dramatic. Drama Criticism and Appreciation*: Britain: Collins Educational.

Hussein, E. N. (1969) *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

_________________ (1971) *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (2009) *Kaptula la Marx*. Nairobi: Vide- Muwa Publishers.

Kiongera, K. (2012) *Mchango wa Vijana katika kuleta Mabadiliko Chanya Katika Tamthilia Teule za Kiswahili*:

Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa.)

Kisiroche, R. (2008) *Sauti ya Mwanamke Dhidi ya Ubabedume*: Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapichwa.)

Madison, D. & Hamera, J. (2005) *The Sage Handbook of Performance Studies.Performance of and Beyond Literature*. www.sagepub.com.

Mazrui, A. (1984) *Kilio Cha Haki*. Nairobi: Marimba Publisher Ltd.

Mazrui, A. na Njogu, K. (2006) *Sudana*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Textbooks Graphics and Publishing.

__________________ (2006) *Migogoro*. Nairobi: JKF.

Mberia, K. (2001) *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers Ltd.

Mohamed, S.A. (1995) *Kunga za Nathari ya Kiswahili Riwaya Tamthilia na Hadithi Fupi.* Nairobi: East Africa Educational Publishers.

__________________ (1995) *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

____________________ (2011) *Kimya Kimya Kimya*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mukobwa, J.M. (1985) *Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthilia Tano za Hussein E.*: Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa.)

Musyoka, M. (1996) *Fani katika Tamthilia za Jay Kitsao*: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapisha.)

Mutswenje, S. (2012) *Taswira ya Mwanamke katika Tamthili mbili za Kiswahili:* Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa.)

Mwedarani, B. (2012) *Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia Mbili za Kiswahili*: Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa.)

Shaaban, R, (1951) *Kusadikika.* Nairobi: Evans Brothers Kenya Ltd.

Shepherd, S. & Wallis, M. (2004) *Drama /Theatre/Performance/ The New Critical Idiom*. New York: Routledge.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* .Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R.M (2003) *Uhakiki wa Tamthilia Historian na Maendeleo yake*. Nairobi: JKF.

Waihiga, K. na Kamau, S. (2002) *Mwongozo wa Kilio cha Haki*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Wamitila, K. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Litho Ltd.

____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

____________ (2008) *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

____________ (2011) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Were, E. (2012) *Fani katika Tamthilia ya Kiswahili*: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa.)

Williams, R. (1968) *Drama In Performance*. London: C.A. Watts & Co. Ltd.

Wilson, E. (1998) *The Theatre Experience*. New York: The McGraw Hill Companies.